# Nipashe

Jumatano Januari 22, 2025 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581929 www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0677 020 710 LIKE & FOLLOW US Nipashe digital

epaper.ippmedia.com Nipashe MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii www.ippmedia.com



**Maduka** 14 yateketea moto, mfanyabiashara apata mshtuko
UKURASA WA 4

**Wenye** ndoto kusaka urais CCM waonywa, wapewa somo
UKURASA WA 4





**Wakili** kesi ya mauaji Katibu wa CCM ataka kasi upelelezi
UKURASA WA 7





VINICIUS JR AWATOA UDENDA WASAUDIA
UKURASA 21


# Hatima ya CHADEMA

• **Hofu** yatanda mpasuko; Lissu asema hajawahi kugombana na Mbowe...

*Ukurasa 2 & 3*



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Taifa, Freeman Mbowe akifurahia jambo na Makamu Mwenyekiti Bara,Tundu Lissu, kabla ya uchaguzi kufanyika, wakati wa Mkutano Mkuu wa chama hicho, Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

UKURASA WA 8


## ACT YAANZA KUTIA NIA KWENYE UBUNGE

SIKU chache baada ya Chama cha ACT-Wazalendo kufungua pazia kwa wanachama wake kutangaza nia kuwania nafasi mbalimbali katika uchaguzi mkuu unaotarajia kufanyika mwishoni mwa mwaka huu, Waziri Kivuli Ofisi ya ...

UKURASA WA 8

## SERIKALI YAAHIDI MAZINGIRA BORA KWA WAFANYABIASHARA

MKUU wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, amesema serikali imejipanga kuendelea kuimarisha mazingira bora kwa wafanyabiashara ili waweze kulipa ...



## Trump aanza kazi, akunjua rasmi makucha

UKURASA 19

# Azuia mwanawe kuzikwa ili apelekwe kanisani kufufuliwa

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

MKAZI wa Mtaa wa Nguzo -Forest, Manispaa ya Morogoro, amezuia mwili wa mtoto wake, Irene Akaro (30), kuzikwa badala yake upelekwe kwenye Kanisa la Ufufuo na Uzima ili aombewe, akiamini hajafariki dunia kwa mapenzi ya Mungu.

Wakati mama huyo akitaka ifanyike hivyo, baba wa mtoto huyo ametaka mwili wa mwanawe uzikwe kwa imani ya Kanisa Katoliki na kusafirishwa kwenda Moshi, Kilimanjaro kwa ajili ya maziko.

Mwandishi wa habari hii alifika nyumbani kwa wazazi hao jana na kukuta sintofahamu hiyo ikiendelea, huku mama wa marehemu ambaye jina lake halijapatikana mara moja akilazimisha kutoka nje ili azungumze na vyombo vya habari wamsaidie mwili wa mwanawe kupelekwa kanisani.

Wakati mama huyo akishikilia msimamo huo, ndugu wengine walijitokeza kuzuia

ENDELEA UKURASA 4


MICHEZO YANGA YAANIKA ILIPOJIKWAA CAF UK.24 MAONI, UK.6

# Hofu yatanda kuibuka mpasuko CHADEMA

**Elizabeth Zaya**

WAJUMBE wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), wameingiwa na hofu ya kuwapo hatari ya chama hicho kupasuka au kuimarika zaidi baada ya kumalizika kwa uchaguzi wa ndani wa kuwapata viongozi.

Walisema hayo jana Dar es Salaam kwa nyakati tofauti wakati wakijiandaa kuwachagua viongozi wa juu wa chama hicho wakiwamo Mwenyekiti na Makamu Wenyeviti Bara na Zanzibar.

Wanachama hao waliiambia Nipashe kuwa haijawahi kutokea tangu chama hicho kianze kufanya uchaguzi wa ndani wa viongozi wakuu kuwa na ushindani mkubwa kiwango hicho.

Wanaogombea nafasi ya uenyekiti ni Freeman Mbowe anayetetea nafasi hiyo, Tundu Lissu ambaye ni Makamu Mwenyekiti hadi jana na Charles Odero.

Kwa nyakati tofauti, wajumbe hao walisema uchaguzi wa mwaka huu umekuwa na mvuto mkali kutokana na kugonganisha vigogo wawili ambao ni nguli na wanaokubalika katika kisiasa.

Baadhi ya wanachama wajumbe wa mkutano huo mkuu walisema hawajawahi kukutana na uchaguzi wenye upinzani ndani ya chama hicho kama ilivyokuwa awamu hiyo.

Mjumbe kutoka Manyara, Regula Mtei, alisema haijawahi kutokea kwenye uchaguzi uliopita kutokea na ushindani mkali kama ilivyotokea katika uchaguzi wa awamu hii.

"Na hii imetokea kwa sababu wamesimama manguli wawili. Uchaguzi huu umeleta mvuto ndani na nje ya CHADEMA kwa sababu ni watu wanaojua siasa, wanafanya siasa kama zinazofanyika duniani," alisema Regula.

Alisema uchaguzi wa mwaka huu hautabiriki kutokana na nguvu kubwa iliyopo kwa pande mbili za wagombea.

"Hatuwezi kutabiri kwa sababu uchaguzi una gharama zake, lakini tunachoamini ni kwamba lolote litakalotokea chama na msingi uliowekwa ndani ya chama utasaidia kukiimarisha tena," alisema.

Mjumbe kutoka mkoa wa Mbeya, Masaga Karoli, alisema: "Mimi nilishiriki uchaguzi wa mwaka 2019 ambao haukuteka hisia za watu lakini huu umeteka hisia nje na ndani ya chama kwa sababu umewakutanisha nguli wawili, wanye mtaji mkubwa wa kisiasa.

"Lakini nimesikiliza hotuba za wagombea. Nimeiona nia ya dhati ya kutuunganisha baada ya uchaguzi isipokuwa wasiwasi wangu upo kwa hawa wapambe wanaounga mkono wagombea maana kuna baadhi wameingia na matokeo yao mfukoni kwamba lazima fulani ashinde. Sasa hao ndio wenye shida kwa sababu ukiingia namna hiyo halafu ikawa ndivyo sivyo, inaweza kukuletea shida."

Mjumbe kutoka Kisesa Mkoa wa Simiyu, Fabian Masunga, alisema ni jambo la busara sana kwa atakayeshinda na atakayeshindwa, hivyo wakubaliane na matokeo na washikane mikono.

"Lissu tunampenda na Mbowe tunampenda na ndiyo wametufanya tufikie hapa leo ila uchaguzi wa leo ni 50/50 tuwe hapa leo na kama CHADEMA itafanikiwa kutoka salama hapa, itakwenda kuwa kubwa zaidi," alisema Masunga.

Mjumbe kutoka Siha, Filbert Mmari, alisema chama hicho kimefanya uchaguzi ambao umeweka historia kutokana na mvuto wake na aina ya watu wanaogombea.

"Hii miamba inayoshiriki uchaguzi imesababisha kuleta historia ambayo haijawahi kutokea ndani ya chama chetu. Hii imesaidia pia kuonesha kwamba demokrasia ndiyo inatakiwa kuwa namna hii. Tunachoombea ni kwamba chama kiendelee kubaki salama kwa sababu sisi wengine hatuna chama kingine cha kwenda," alisema Mmari.

Mjumbe kutoka Mjini Unguja, Abeid Haji Abeid, alisema uchaguzi uko vizuri isipokuwa anachokiona ni wapambe au ushabiki wa nje kuwa mkubwa na kusababisha taharuki.

Mjumbe kutoka Pemba, Habib Ali Khamis, alisema uchaguzi wa sasa umewafundisha jambo kubwa na kwamba kuanzia kundi la wajumbe wachache wa mkutano ambao ndio wanawaaminisha wengine wasio wapiga kura lakini anaamini chama hicho kitatoka salama.

Naye mjumbe kutoka Bunda, Samson Kandole, alisema huko alikotoka wanachama wamemtuma na kumpatia maelekezo mtu wa kumchagua na kwamba endapo matokeo hayatakuwa sawa na yule waliyemtaka, wako tayari kuacha chama na kuahirisha nafasi zote walizokuwa wamepanga kugombea kupeperusha chama hicho katika uchaguzi mkuu ujao wa Rais, Wabunge na Madiwani ikiwamo za ubunge na udiwani.

Kamuli Elias kutoka Bunda, alisema chama kina wakati mgumu kuhakikisha kinavuka salama baada ya uchaguzi.

Kabla ya kuanza kupiga kura, Katibu Mkuu wa CHADEMA, John alitangaza kuwa Lissu kumteua Godbless Lema kuwa wakala wake.

Mnyika pia alitangaza kufanyika uhakiki wa wajumbe, huku kukiwa na madai ya kuwamo ukumbini watu wasiokuwa wajumbe wa Mkutano Mkuu. Waliothibitika kutokuwa wajumbe, waliondolewa ukumbini.

***Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga/ sms / WhatsApp : +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***



Wajumbe wakiwa kwenye Mkutano Mkuu wa chama hicho, Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Polisi watanda Mlimani City

**Na Halfan Chusi**

JESHI la Polisi liliimarisha ulinzi Mlimani City, Dar es Salaam ulikofanyika Mkutano Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) huku magari ya jeshi hilo yakiwa yameegeshwa kwenye eneo hilo la kibiashara.

Wakati polisi wakiwa wametanda kwenye eneo hilo, wafuasi wa chama hicho walikuwa wamefurika nje na ndani ya jengo hilo wakiwa wameshika mabango ya wagombea wanaowania nafasi mbalimbali.

Wafuasi hao wa pande mbalimbali walisikika wakiimba nyimbo mbalimbali za kuwanadi wagombea wao huku wakiwa wameshika mabango yenye sura zao.

Baadhi ya wafuasi hao walisikika wakiimba: "Heche... Lissu... Heche... Lissu... Heche... Lissu..." wakiwa na maana wanamuunga mkono Lissu na Heche katika uchaguzi huo.

Ulinzi pia uliimarishwa kwenye milango ya kuingia ukumbini, hakuna aliyeruhusiwa kuingia pasi na kuwa na kadi maalum ya mwaliko, wahusika wakidai kuwa walifanya hivyo ili kudhibiti mamluki katika uchaguzi huo.

Pamoja na hayo, ubishani mkali ulizuka nje ya viunga vya ukumbi, pande mbili zikirushiana maneno na tambo -- upande mmoja ukitamba Lissu atashinda, na mwingine ukitamba Mbowe atashinda.

# ...Lissu atangaza msimamo kuhusu matokeo ya uchaguzi

**Na Restuta James**

KABLA ya uchaguzi wa viongozi wa kitaifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), mgombea uenyekiti, Tundu Lissu alizima uvumi wa mitandaoni kwamba atakihama chama hicho asiposhinda.

Alisema yuko tayari kupokea matokeo yoyote na kwamba hata akishindwa atabakia ndani ya chama hicho.

Alisema hayo Dar es Salaam jana wakati akitoa salamu zake mbele ya wajumbe wa Mkutano Mkuu wa chama hicho uliofanya uchaguzi wa viongozi wa kitaifa na wajumbe wa Kamati Kuu.

Lissu alisema pamoja na kutofautiana na Mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe kwa misimamo lakini hawajawahi kugombana.

"Ndugu zangu na wajumbe wenzangu, huu ni mkutano wangu wa kwanza ndani ya chama ninaouhudhuria tangu mwaka 2014. Hii ni kwa sababu katika Mkutano Mkuu wa 2019, nilikuwa ninatibiwa Ubelgiji kufuatia tukio la jaribio la mauaji dhidi yangu Septemba 7, 2017," alisema.

Alikumbusha kuwa pamoja na kwamba alikuwa kitandani, aliomba kura ya kuwa Makamu Mwenyekiti Bara na wajumbe walimchagua kwa asilimia 98.8 ya kura 941 zilizopigwa siku hiyo.

Lissu alisema kuwa mwaka 2020 wajumbe hao walimpitisha kwa asilimia 100 ya kura na kumwidhinisha kuwa mgombea urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Alisema huo ni ushahidi kwamba wajumbe walimchagua kutokana na imani yao kwenye uwezo wake.

"Niseme nini kwenu! Kwa watu ambao mmenipenda kiasi hiki, watu ambao mmenipa fadhila nyingi... vyovyote itakavyokuwa leo (jana), tutakuwa pamoja kujenga chama chetu," alisema Lissu huku akishangiliwa na wajumbe.

"Leo ninamaliza miaka yangu mitano, ninapenda kuamini nimewatumikia, nimekitumikia chama chetu na nimewatumikia wananchi wetu kwa namna ambayo tuna haki ya kujivunia," alisema.

Kuhusu uhusiano wake na Mbowe, Lissu alisema amekuwa naye bega kwa bega kwa miaka 20 na hajawahi kugombana naye.

Lissu alisema: "Tunaweza kuwa tumetofautiana kimsimamo, lakini hatujawahi kugombana".

Alisema anaamini kwamba uhusiano wake na Mbowe utaendelea kama zamani baada ya uchaguzi huo.

"Nitayasema hayo hayo kwa viongozi wenzangu wa chama. Tunaweza kuwa tumetofautiana kimsimamo, lakini hatujawahi kugombana. Ninaomba nitumie nafasi hii kuwashukuru nyote kwa miaka hii 20 ya utumishi wangu ndani ya chama chetu," alisema.

Lissu alisema kuwa uamuzi wowote utakaofanywa na wajumbe wa chama hicho ni sehemu ya ujenzi wa chama, naye ni muumini wa ujenzi wa chama hicho.

**WAJUMBE WAMSHANGILIA**

Alipoitwa na Katibu Mkuu wa chama hicho, John Mnyika kutoa salamu zake, wajumbe walilipuka kwa shangwe wakiimba "Lissu... Lissu... Lissu..."

Lissu alichuana na Mbowe na Charles Odero kwenye nafasi ya uenyekiti. Nafasi nyingine iliyokuwa na mchuano mkali katika uchaguzi huo ni ya Makamu Mwenyekiti Tanzania Bara, washindani wakiwa ni John Heche anayemuunga mkono Lissu na Ezekia Wenje aliye upande wa Mbowe.

Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, wanaogombea Umakamu Mwenyekiti wa Chama, ni Hafidh Ali Saleh, Suleiman Makame Issa, Said Issa Mohammed na Said Mzee Said.

## HABARI KITAIFA

## Moshi mweupe Bahati Nasibu ya Taifa

**Na Mwandishi Wetu**

BAHATI Nasibu ya Taifa Tanzania iko mbioni kuanza rasmi, Naibu Waziri wa Fedha, Hamad Chande, akitangaza kampuni itakayosimamia uendeshaji wake.

Katika mkutano na wahariri wa vyombo vya habari jijini Dar es Salaam jana, Naibu Waziri Chande alisema kampuni ya ITHUBA itaendesha michezo ya bahati nasibu kwa lengo la kuleta mapinduzi katika sekta hiyo, kuchochea maendeleo ya kitaifa na kutoa fursa kwa kila mtanzania kushiriki.

"Leo (jana) ni siku ya kihistoria kwa Tanzania," alisema Chande wakati wa hotuba yake. Kwa kumkaribisha rasmi mwendeshaji huyu wa Bahati Nasibu ya Taifa, tunatoa kipaumbele katika suala zima la uvumbuzi, uaminifu na uwazi huku tukileta jukwaa litakalochochea ukuaji wa uchumi, ajira mpya na miradi ya maendeleo ya kitaifa kwa ajili ya kuinua maisha ya wananchi."

Alisema Bahati Nasibu ya Kitaifa itakuwa na mkusanyiko wa michezo mbalimbali ya kuvutia iliyoundwa mahususi kwa ajili ya kuwashirikisha na kuwaburudisha watanzania. Tiketi zinaanzia bei ya Sh. 100 kuhakikisha kila mtu anaweza kushiriki.

"Kila tiketi itakayouzwa itachangia kuboresha michezo, elimu, na miradi ya kijamii," alisema Chande. "Bahati Nasibu ya Taifa ni mfano wa jinsi michezo ya kubahatisha inavyoweza kutumika kama chombo cha maendeleo endelevu huku ikiwaletea washiriki furaha."

Ofisa Mtendaji Mkuu wa ITHUBA Group, Charmaine Mabuza, alisisitiza dhamira ya kampuni hiyo katika maendeleo ya Tanzania, akiahidi kushirikiana na Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT) kuendesha Bahati Nasibu ya Taifa.

"Bahati Nasibu hii si tu kuhusu michezo bali pia ni sehemu ya kuinua jamii zetu na kuwekeza katika mustakabali bora wa Tanzania," alisema.

Balozi Modest Mero, Mwenyekiti wa GBT, alibainisha umuhimu wa uadilifu katika mpango huo, akisema uwajibikaji kimaadili na uvumbuzi unafanya kampuni mwendeshaji kuwa mshirika bora.

Alisema GBT itahakikisha Bahati Nasibu ya Taifa inafanya kazi kwa uwazi na uaminifu kama jukwaa salama linalochangia malengo ya kiuchumi ya Tanzania.

Aliongeza kuwa Bahati Nasibu ya Taifa inatarajiwa kuleta mabadiliko makubwa katika sekta ya michezo ya kubahatisha nchini. Mapato ya tiketi yatatumika kufadhili maendeleo ya michezo katika ngazi ya msingi, uwezeshaji vijana na miradi muhimu ya kijamii, kuimarisha jukumu la Bahati Nasibu ya Taifa kama chombo cha maendeleo ya kijamii.

Katika uendeshaji Bahati Nasibu ya Taifa, zaidi ya Dola za Marekani milioni 3.5 zimetengwa kwa ajili ya masoko na matangazo katika vyombo vya habari, ikijumuisha fursa za kipekee za maudhui.




Baadhi ya wanachama wa CHADEMA, wakiwa na mabango ya kuwapigia kampeni wagombea wao, nje ya Mkutano Mkuu wa chama hicho, Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mbowe awapa kibarua viongozi wajao

**Na Restuta James**

ALIYEKUWA Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na mgombea wa nafasi hiyo katika uchaguzi wa jana, Freeman Mbowe, amewasihi viongozi watakaoshika nyadhifa, wakijenge chama katika misingi ya maadili na nidhamu.

Akifugua mkutano wa chama hicho jana, Mbowe alisema: "Tumeona minyukano kadha wa kadha. Jambo hili si sifa, ni aibu ya chama ambayo hatupaswi kuliendeleza. Yeyote atakayechukua kijiti cha kukiongoza chama hiki, Kamati Kuu ijayo, wajibu wa kwanza tunaowaachia warithi wa mikoba yetu ni kurejesha nidhamu, kurejesha kuheshimu maadili ya chama hiki na kuhakikisha hakuna matusi ndani ya CHADEMA," alisema.

Mbowe alisema wajibu wa viongozi wajao ni kuhakikisha kila mwana CHADEMA anamjenga mwenzake na kuimarisha chama kama taasisi.

"Ambaye atakataa kukubaliana na msimamo huu, huyo si mwenzetu. Niwashauri na kuwasihi sana, uwapo wetu leo unaakisi maumivu na jasho la watu walioumia kuijenga CHADEMA," alisema.

Alisema minyukano, kubezana na kudhalilishana haupaswi kuwa utamaduni wa CHADEMA kwa kuwa inabomoa haiba na heshima ya chama, hivyo kusisitiza kuwa wanachama, viongozi na wafuasi wa CHADEMA wana dhamana ya kukilinda chama kwa gharama yoyote.

"Chama hiki hatutakiruhusu kwa namna yoyote eti kwa sababu pengine kura za Mbowe, Lissu au Odero hazikutosha, uchaguzi huu haupaswi kuwa vita bali unapaswa kuwa furaha ya ujenzi wa demokrasia," alisema.

Alisema kuna watu wanadhani CHADEMA itamaliza uchaguzi ikiwa vipande vipande, jambo ambalo alisema anaamini halitatokea bali itamaliza ikiwa imara zaidi akitumia kaulimbiu ya 'stronger together'.

Kaulimbiu ya 'stronger together' imeletwa ili kuwakumbusha wanachama kwamba pamoja na presha iliyojengwa wakati wa maandalizi ya mkutano na uchaguzi huo, wanapaswa kuendelea kuwa pamoja.

"Katikati ya tofauti zetu, bado umoja wetu ndio nguvu yetu. Katikati ya mitazamo tofauti, bado kwa pamoja tuna nguvu...kauli hii ni kielelezo cha utayari wa Kamati Kuu kwamba pamoja na tofauti zetu tukilinde chama chetu, heshima ya chama chetu ilindwe.

"Chama hiki leo kimebeba ndoto ya taifa, sio ndoto ya Mbowe wala ndoto ya viongozi wa meza kuu. Wako Watanzania maelfu ambao hawana kadi za Chadema lakini wanaamini kesho ya watoto wao itatokana na Chadema," alisema.

Mbowe alisema ni jukumu la wanachama na viongozi ngazi zote kulinda heshima na nguvu CHADEMA, kwa kukijenga katika maadili na nidhamu.

Alisema chama hicho kilizaliwa Januari 21, 1993 kwa kupata usajili wa kudumu na kwamba uchaguzi unafanyika kama sehemu ya maadhimisho ya miaka 32 ya uhai wake.

Mwonekano wa sasa wa chama hicho, alisema ni safari ya miaka 32 yenye mchanganyiko wa hisia za maumivu, jasho na damu. Alisema CHADEMA kimefanikiwa kuwa chama kikubwa ndani ya nchi kutokana na 'makamanda' walisimama imara kukilinda kwa nguvu na akili.

"Wako wengine tulioanza nao safari hii, hawakuweza kuiona siku ya leo, nikianza kuhesabu waasisi kama wako walio hai hawazidi asilimia tano," alisema.

Mbowe alisema chama hicho kimejengwa na wanachama wote wa CHADEMA hatua kwa hatua na kwamba sio nguvu za viongozi.

"Ndio maana tunasema siku zote chama hiki ni mpango wa Mungu. Dhoruba na mishale tuliyopitia, leo tuko hapa kwa sababu Mungu anakusudi na chama hiki kwa sababu ya Tanzania.

"Mtakaopewa mikoba ya chama hicho lazima mkarekebishe, inawezekana tukavumilia matusi kipindi hiki cha chaguzi lakini msingi wa CHADEMA haupaswi kuwa matusi," alisema.

Mbowe amesema CHADEMA itamaliza uchaguzi wakiwa wamoja na kwamba uchaguzi huo sio vita.

VISIT
ENTRY FREE
INTL TRADE EXHIBITION ON AGRO & POULTRY - GRAINS
EXHIBITORS FROM AROUND 17 COUNTRIES
AGRO & POULTRY 2025
Products on Display:
ANIMAL HEALTH | ANIMAL FEEDS | DAIRY PRODUCTS
FEEDS MACHINERY | FEEDS ADDIVITES
Grains Africa 2025
Products on Display:
FLOUR & PASTA ADDITIVES | BREAK ADDITIVES
FEED QUALITY CONTROL DEVICES | WHEAT & FLOUR ANALYSERS
SILOS | FRESH FRUITS PROCESSING SYSTEM
FEEDS MILLS | FLOUR MILLS | MILLILNG PLANTS
GRAINS PROCESSING SYSTEM
Date & Venue
23-25 January 2025
Diamond Jubilee Hall, Dar-Es-Salaam - Tanzania
Timing
10:00 AM TO 6:00 PM
For more info, Please Call
0758 571652 / 0656 482557

# Azuia mwanawe kuzikwa ili apelekwe kanisani kufufuliwa

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

MKAZI wa Mtaa wa Nguzo -Forest, Manispaa ya Morogoro, amezuia mwili wa mtoto wake, Irene Akaro (30), kuzikwa badala yake upelekwe kwenye Kanisa la Ufufuo na Uzima ili aombewe, akiamini hajafariki dunia kwa mapenzi ya Mungu.

Wakati mama huyo akitaka ifanyike hivyo, baba wa mtoto huyo ametaka mwili wa mwanawe uzikwe kwa imani ya Kanisa Katoliki na kusafirishwa kwenda Moshi, Kilimanjaro kwa ajili ya maziko.

Mwandishi wa habari hii alifika nyumbani kwa wazazi hao jana na kukuta sintofahamu hiyo ikiendelea, huku mama wa marehemu ambaye jina lake halijapatikana mara moja akilazimisha kutoka nje ili azungumze na vyombo vya habari wamsaidie mwili wa mwanawe kupelekwa kanisani.

Wakati mama huyo akishikilia msimamo huo, ndugu wengine walijitokeza kuzuia wakidai suala hilo liachiwe familia kwa vile ni la kifamilia.

Mwanamke huyo anayedaiwa kutokula chakula tangu juzi alipopata taarifa za kifo cha binti yake, alitafuta usafiri wa jirani na kukimbilia kwenye kanisa hilo lililoko Mkundi katika Manispaa ya Morogoro kwa madai muda ulizidi kwenda.

Mama huyo anadai kuwa anaamini kifo cha mwanawe si cha kawaida na anakihusisha na kesi ya madai iliyoko mahakamani ambapo mwanawe alimfungulia mwenzake aliyekuwa akimdai kwa muda mrefu.

"Hii ni imani yangu, wanipe kibali nimpeleke mwanangu kanisani akaombewe. Kuna mtoto alipata vipele nikashauri yachukuliwe majani ya chunga asuguliwe na atapona na kweli akapona. Hii pia naamini mtoto akipelekwa kwenye maombi ataamka kwani hajafa," alisisitiza mama huyo aliyekuwa akidhibitiwa kuzungumza na waandishi wa habari.

Mtoto wa kiume katika familia hiyo ambaye ni kaka wa marehemu aliyekuwa akidhibiti hata kamera kupiga picha, alisema wangezungumza suala hilo baada ya vikao vya kifamilia na kwamba walisharidhia ombi la mama yao ili kumsaidia kiafya.

Hata hivyo, viongozi wa Kanisa Katoliki waliokuwapo eneo la tukio, walisema kama mwili ungepelekwa kwenye makanisa ya kipentekoste, wasingehusika tena na maziko, jambo ambalo liliwatia simanzi wanafamilia upande wa baba walioona kwa kufanya hivyo wangekwenda kinyume cha imani.

Baadhi ya ndugu upande wa baba waliokuwa wakirekodiwa huku wakikataa kutaja majina, walisema wanachotaka familia ni viongozi wa kipentekoste kwenda kufanya maombi kwa mwili huo katika chumba cha kuhifadhi maiti cha Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro, ulikohifadhiwa au nyumbani kwa wazazi, jambo ambalo mama huyo aligoma akidai mchungaji anachotaka ni mwili upelekwe kanisani.

Mmoja wa viongozi wa madhehebu ya Pentekoste, Askofu Mkuu Willy Mpala wa Kanisa la The Light of Christ Mobile lililoko Lukobe, Mkundi, akizungumza msibani hapo, alisema wanachoamini kama makanisa ya kipentekoste ni ufufuo na huenda mama wa marehemu alipewa ufunuo kuwa binti yake akiombewa angefufuka na atafufuka kweli.

"Sisi hatuamini katika ibada ya maziko. Tunaamini kwenye maombi na ufufuo. Huyu binti alizaliwa kwenye imani ya katoliki, baadaye akaja kwetu, akabatizwa na akawa anasali na kufanya matendo mengi mema ikiwamo kusaidia yatima.

"Baadaye aliondoka na kabla ya umauti, alirudi tena kanisani kwake kwa zamani Katoliki lakini mama yake ameamua apelekwe Kanisa la Ufufuo na Uzima akaombewe, hivyo asikilizwe," alisema Askofu huyo.

Mmoja wa majirani, Mbaraka Athumani, alisema anaamini kila mtu anakufa na huyo mtoto ingawa walimpenda na kushirikiana naye kwa mengi, amefariki dunia, hivyo ndugu wakubali kumzika, akapumzike na imani yake na kusisitiza kuwa hawezi kufufuka tena.

"Ninachoomba azikwe Morogoro na asisafirishwe ili wengi tupate nafasi ya kumzika. Tumeishi naye vizuri akiwa hai, ametuuzia maziwa hapa, tumecheka na kufurahi naye," alisema jirani.

Hadi mwandishi wa habari hii anaondoka eneo la tukio, bado kulikuwa hakuna utaratibu wa wazi ni hatua gani zaidi zingeendelea kuchukuliwa na familia kuhusu mwili wa Irene aliyedaiwa pia kujihusisha na biashara ndogo ndogo zikiwamo za viatu eneo la Luna, Manispaa ya Morogoro.

# Moto wateketeza maduka 14 Dodoma

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MADUKA 14 ya bidhaa mbalimbali jijini hapa, yameteketea kwa moto katika Mtaa wa Mwangaza, ulioko barabara ya nane baada ya moto kuzuka huku chanzo kikisadikiwa kuwa ni miundombinu chakavu ya nyaya za umeme.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Dodoma, Rehema Menda, alisema katika ajali hiyo iliyotokea jana, hakuna aliyepoteza maisha, isipokuwa mmiliki mmoja wa duka aliyefahamika kwa jina moja la Kimaro, alipata mshtuko na kupelekwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa baada ya moto huo kuzimwa, ikiwamo kuokoa baadhi ya mali zilizokuwa ndani ya maduka hayo, alisema jeshi hilo linaendelea na uchunguzi kubaini chanzo cha ajali hiyo.

Menda alisema tukio hilo lililotokea jana majira ya saa 1:26 asubuhi kutokana na cheche za moto zilizotoka katika moja ya maduka yaliyoko kwenye nyumba hiyo ndipo moto ukaanza kusambaa kwa kasi kwenda duka moja hadi lingine, hivyo na kusababisha taharuki katika eneo hilo.

Kamanda Menda alisema jeshi hilo kwa kiasi kikubwa kuokoa mali zilizokuwa ndani ya maduka hayo, huku nyingine zikiteketea kutokana na moto mkali uliokuwa ukisambaa kutokana na vitu vilivyopo ndani ya maduka hayo kushika moto.

"Tunawashukuru wananchi kutokana na kutoa taarifa ya moto huu mapema, lakini pia niwaombe muwe na haraka ya kutoa taarifa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kabla ya athari kubwa ya moto kusambaa," alisema.

Pia alisema kusambaa kwa kasi kwa moto huo kulitokana na bidhaa ambazo zimehifadhiwa ndani ya maduka hayo, kama vile magodoro, matairi, nguo na vitu vingine ambavyo ni chakula cha moto.

Kadhalika, aliwataka wamiliki wa nyumba ambazo wamepanga maduka ya biashara pamoja na makazi, kuwa na utaratibu wa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye nyaya za umeme ili kuepuka majanga kama hayo.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, akizungumza kwenye eneo la tukio hilo, aliwataka wafanyabiashara na wamiliki wa maduka kuwa na utaratibu wa kukata bima za majanga ambazo zitawasaidia endapo watakumbwa na matatizo mbalimbali katika biashara zao.



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Fadhili Maganya, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu kuunga mkono uamuzi wa mkutano mkuu wa chama hicho, kuwapitisha Rais Samia Suluhu Hassan na Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi kuwa wagombea urais kwenye uchaguzi mkuu mwaka huu. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Wenye ndoto kuwa Rais CCM waonywa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Fadhili Maganya, amesema baada ya Mkutano Mkuu Maalum wa chama hicho, kupitisha majina ya wagombea urais, kwenye uchaguzi mkuu mwaka huu, jambo hilo limefungwa rasmi.

Aidha, amesema kutokana na hali hiyo, mwanachama yeyote ambaye anaona hawezi kuishi bila urais basi anapaswa kwenda kuutafuta sehemu nyingine na si ndani ya CCM.

Maganya alisema hayo jana jijini hapa, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uamuzi wa Mkutano Mkuu Maalum wa CCM kuwapitisha Rais Samia Suluhu Hassan na Dk. Hussein Ali Mwinyi kuwa wagombea wa nafasi ya urais kwa Tanzania na Zanzibar.

"Jumuiya ya Wazazi wa Chama Cha Mapinduzi inaunga mkono uamuzi wa mkutano mkuu ulifanyika jijini hapa mwishoni mwa wiki iliyopita na kwa uamuzi huo, nitoe rai kwa wanachama wote wa CCM nchini kuwaunga mkono wagombea hawa na kuwatafutia kura za kutosha.

"Lakini kama kuna mwanachama ambaye yeye anaona kuwa hawezi kuishi bila urais, nafasi hiyo ndani ya CCM haipo tena labda akatafute urais kwenye taasisi zingine au kwenye vyama vya michezo huku pia ziko nafasi za urais, unaoanza na R ndogo," alisema Maganya.

Akizungumzia kuhusu chama hicho kuwahi kupitisha majina ya wagombea urais, alisema hali hiyo inatokana na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi uliofanywa na serikali zote mbili ambao umewaridhisha wajumbe wa mkutano mkuu.

"Sisi tumeamua kupitisha wagombea wetu mapema na hakuna aliyewahi kulaumiwa kwa kuwahi lakini anayechelewa analaumiwa, hivyo CCM ni chama kikubwa ambacho kimekomaa na uamuzi wake si wa kubahatisha tofauti na vyama vingine," alisema.

Aidha, aliagiza jumuiya hiyo kuanzia ngazi za chini hadi taifa, kuwaunga mkono wagombea urais walioteuliwa na mkutano mkuu na kuhakikisha wanawatafutia kura ili chama kuendelea kuongoza nchi.

Mkutano Mkuu Maalumu wa CCM, ulioketi jijini Dodoma Januari 18 na 19, mwaka huu, ulipitisha azimio kuwa Rais Samia Suluhu Hassan wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi wa Zanzibar kuwa wagombea wa nafasi ya urais katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

TANGAZO

# Bank of India (Tanzania) Ltd.

**Fully owned subsidiary of Bank of India (Public Sector Bank)** *Relationships beyond banking*

## DISCLOSURES MADE UNDER REGULATION 11 OF BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATIONS, 2014 AND CONSUMER PROTECTION REGULATION, 2019 MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES (GHARAMA ZA HUDUMA ZETU)

### Service Charges (Exclusive of VAT and Government Levy on Digital Transactions)
### (The applicable VAT (Value added Tax) and Govt Levy on digital Transaction to be collected during the collection of service charges)

### A. REMITTANCE –OUTWARD

| Sr. No. | Item | Charge in TZS or Equivalent to TZS |
|---|---|---|
| **TISS Remittance** (Only for A/c holders – Not permitted for non a/c holders) | Remittance -TZS or TZS Equivalent Transaction value | |
| | Between TZS 1 to 10 million | 2,000 |
| | Between TZS 10 million to 50 million | 5,000 |
| | Above TZS 50 million | 10,000 |
| | | |
| | | |
| **TIPS AND TACH** | Transaction value | |
| | Between TZS 1-TZS 50,000 | 500 |
| | Between TZS 50,001-TZS 500,000 | 1,000 |
| | Between. TZS 500,001- 5,000,000 | 1,500 |
| | Between. TZS 5,000,001- 20,000,000 | 2,500 |
| | | |
| | | |
| **Other Outward Remittance** | 1USD up to 6,000 | USD 15 |
| | USD 6,001 – 10,000 | USD 30 |
| | Above USD10,000 | @ 0.35% Maximum USD 75 |
| Tracer Charges | Irrespective of Amount | USD 30 |
| Recall back funds charges | Irrespective of Amount | USD 30 |

### B. REMITTANCE –INWARD

| Sr. No. | Item | Charge |
|---|---|---|
| (Only for A/c holders – Not permitted for non a/c holders) | From inside Tanzania (TISS, TIPS AND TACH) | Free |
| | From outside Tanzania: as under | |
| | For Current /Overdraft Accounts | 0.35% of inwards remittance Minimum USD 18 Maximum USD 70. |
| | For Saving Accounts | |
| | USD 0 up to USD 100 | Free |
| | USD 101 up to USD 500 | USD 10 |
| | Above USD 500 | USD 18 |

### C. DEPOSIT AND RELATED SERVICES

| Item | TZS A/c | USD A/c |
|---|---|---|
| **Saving Account :-** | | |
| Cash withdrawal per day –Free of charge, up to amount | TZS 25 Mn | USD 2000 |
| Cash withdrawal charges over USD 2,000 to USD 5000 per day | -- | 0.25% of withdraw amount |
| Cash withdrawal charges over USD 5,000 per day | -- | 0.60% of withdraw amount |
| Cash withdrawal charges over TZS 25 Mn per day | 0.10% of withdrawal amount | |
| Cash Deposit charges over USD 5,000 per day | -- | 0.60% of deposited amount |
| Cash deposit charges for small currency USD notes ranging from USD 1 to USD 20, irrespective of amount deposited (i.e. both for below and above USD 5,000) | -- | 12% (Min USD 1) of the aggregate small currency amount |
| **Current Account:-** | | |
| Cash withdrawal per day –Free of charge, up to amount | TZS 25 Mn | USD 5000 |
| Cash withdrawal charges over USD 5,000 per day | -- | 0.60% of withdrawal amount |
| Cash withdrawal charges over TZS 25.00 Mn per day | 0.15% of withdrawal amount | -- |
| Cash deposit charges over USD 10,000 per day | | 0.60% of deposit |
| **Maintenance of minimum balance: -** | | |
| For Saving Account-Without Cheque Book Facility | TZS 50,000 | USD 50 |
| With Cheque Book Facility | TZS 200,000 | USD 200 |
| For Current Account | TZS 200,000 | USD 200 |
| **Minimum balance charges (in case of non-maintenance of minimum balance)** | | |
| Saving Account - Without cheque book | TZS 900 p.m | USD 4 p.m |
| With cheque book | TZS 3600 pm | USD 15 p.m |
| Current Account- | TZS 20,000 p.m | USD 15 p.m |

### D. Other Common Charges

| Item | Charges | |
|---|---|---|
| | TZS A/c | USD A/c |
| Stop Payment Instructions | TZS 35,000 | USD 28 |
| Regular statement of a/c (Monthly) | Free | Free |
| Interim/additional statement | TZS 1500 per page | USD 1.50 per page |
| Issue of bankers' cheque | TZS 40,000 | USD 30 |
| Cancellation of bankers cheque/DD | TZS 20,000 | USD 15 |
| Issue of Duplicate Bankers cheque/Demand Draft/ Duplicate FDR | TZS 30,000 | USD 20 |
| Application charge for Treasury Bond | TZS 100,000 | USD Equivalent to TZS 100,000 |
| Issue of Balance certificate (Saving Account) | TZS 20,000 | USD Equivalent to TZS 20,000 |
| Issue of Balance certificate (Current Account) | TZS 50,000 | USD Equivalent to TZS 50,000 |
| Signature verification and Photo Attestation charges for Domestic A/c Holders | TZS 10,000 | USD Equivalent to TZS 10,000 |
| Verification of Documents such as KYC Documents along with verification of Photo and Signature of Customer Mentioned account with Bank of India- in India /Overseas | TZS 25,000 | USD Equivalent to TZS 25,000 |
| Savings bank customer Identification card- One time | TZS 20,000 | USD 10 |
| Dormant a/c Activation Per Activation Fees | Individual TZS 5,000 Corporate | Individual USD 3 Corporate |
| | TZS 12,000 | USD 6 |
| Account Freezing/un freezing Charges | Free | Free |
| SMS Alert facility | Free | Free |
| Email Alert Facility | Free | Free |
| Monthly Statement on Registered Email | Free | Free |
| Balance Inquiry (Over the Counter) | Free | Free |
| Charges for Deletion of Decease Person Name from the Saving Account | Free | Free |
| Charges for Addition/modification Account such as Change in respect of Corporate A/c | TZS 20,000 | USD 10 |
| Updating of Mobile No. in A/c (SB,CD,OD) | Free | Free |
| Change /Modification in Address (SB,CD,OD) | Free | Free |
| Issuance of No Dues Certificate for Non-Borrowers. | TZS 10,000 | USD 7 |
| Ledger Folio Charges per Folio (40 lines per Folio) only for Current and Overdraft Accounts | TZS 6,000 per Folio | USD 4 per Folio |
| Postages/Courier Charges Inland/Foreign | TZS 30,000 or actual charges whichever is higher | USD Equivalent to TZS 30,000 |

### E. CLEARING SERVICES

| Item | Charge/Fees | |
|---|---|---|
| | TZS A/c | USD A/c |
| Within walking distance-1 km | TZS 70,000 | USD 45 |
| Far off distance –more than 1 km | TZS 95,000 | USD 65 |
| Cheque returned charges –financial reasons (inward/outward) | TZS 70,000 | USD 55 |
| Inward/outward cheque collection - USD | 0.60% Min comm.18 postages 90 | 0.60% Min comm.18 postages 90 |

### F. CREDIT MATTERS

| Charge/Fees | | |
|---|---|---|
| **Proposal Processing Charges: -** | | |
| New Overdraft/Term Loan/Demand Loan | 1.50% of sanctioned limit (Regular Limit – 1.50% for 12 Months) | |
| TOD/TOL/ADHOC | Proportionate to 1.50% for TOL/TOD/ADHOC Period minimum USD 60 | |
| New NFB BG/LC Facility | 1.50% of sanctioned limit (Regular Limit – 1.50% for 12 Months) | |
| Review of Overdraft Limit | 1.50% on entire sanctioned amount. | |
| Review of Term Loan Demand Loan Personal Loan Vehicle Loan Loan Against Property Etc. | 0.15% maximum USD 600 or TZS 1.20Mn on the reviewed amount and 1.50% on the additional Term Loan /Demand Loan amount. | |
| Schematic Lending up to 36 months/Staff Loan | Nil | |
| Prepayment charges | 2.50% of the prepaid loan amount. | |
| Documentation charges for New Overdraft Limit/Term Loan/Demand Loan/Non Fund base Limit | Actuals as per advocate Bill + 0.30% handling charges<br>1) No Documents charges would be applicable for TOD/TOL/ADHOC Limit, however actual expenses if any to be recovered.<br>2) Documentation charges also NOT Recoverable for the Loan/Overdraft against FDR. | |
| Charges for Amendments/Modification of Sanction Terms | 0.25% on the sanctioned limit<br>**We enumerate the illustrative instances of Modification in Terms and Conditions to be effected at the request of the Borrower where this charge will be levied: -**<br>1) Substitution of Collateral Securities/Personal Guarantee<br>2) Release of Personal Guarantee/Collateral Security.<br>3) Interchangeability of limits.<br>4) Change in project/items of Machinery<br>5) Ceding of charges on assets(Pari-Passu)<br>6) Restructuring, Replacement of Loans/ Deferment of Loan installments.<br>7) Approvals for mergers & amalgamations.<br>8) Any other miscellaneous credit related approvals. | |
| Revalidation of Sanction | **25% of Applicable PPC Charges on Overdraft Limit/Term Loan/Demand Loan** | |
| Lead bank Charges | **USD 1000 or equivalent in TZS per annum/one time** | |
| Fee for Opening Escrow/TRA A/cs (Trust and Retention A/cs) | **Where**<br>**We are Lead bank: Nil**<br>**We are Not Lead Bank:**<br>USD 500 or equivalent in TZS per annum/one time | |
| Charges for Supplying copies of Loaning Documents to Customer. | First instance: Free<br>**USD 10 or equivalent in TZS for further requirement.** | |
| Non/Delayed Submission of Audited Financial Statements of the Company OR wherever applicable | **USD 100 or equivalent in TZS per month or part thereof**<br>**Note:-**Audited Financial statements of the firm/company within 6 months from closure of Financial Year or as approved by TRA for the relevant year. | |
| Inspection charge | **TZS 50,000** or equivalent to USD per visit /inspection or at least once in quarter whichever is higher.<br>**Note:-**<br>1) Out of Pocket Expenses to be recovered additionally along with regular inspection charges wherever applicable<br>**2) Project Monitoring Inspection Charges/Technical Due Diligence Inspection charges:** Considering the fact that this inspection is proposed for safeguarding banks Interest, normal inspection charges besides travelling, boarding/lodging expenses are to be recovered from the borrower. | |
| Issuance of No objection certificate (NOC) | **USD 100 or equivalent in TZS** | |
| 1st party/3rd party Overdraft/Loan against deposit of our Bank (BOITL) | Waiver of Processing & Documentation charge. | |
| Overdraft/Term Loan/Demand Loan Conversion Charges (Currency Conversion) | For Overdraft account 0.50% of Sanction Limit.<br>For Term Loan/Demand Loan 0.50% of O/s Amount | |
| Earmarking of Limits | **USD 500 or equivalent in TZS per annum** | |
| Non Compliance of Sanction terms/Commitment charges | **1.00% additional Penal Interest to be charge till compliance of Sanction terms** | |
| **D&B/ Other Credit Information Search for per Borrowal a/c (New/Additional/Review of limit)** | | |
| Up to TZS 20 Mn/USD 10,000 (Only for new and additional Limit. **Review – No charge**) | USD Facility<br>USD 5 | TZS Facility<br>TZS 5,000 |
| Over USD 10,000 to USD 50,000/ Over TZS 20 Mn up to TZS 100 Mn | USD 10 | TZS 20,000 |
| Over USD 50,000/TZS 100 Mn | USD 50 | TZS 100,000 |
| D&B Search for non-Borrower, on request | USD 50 | TZS 100,000 |
| Charges for Furnishing copy of Credit Information report obtained from CIC | **TZS 20,000** | **USD 10** |

| | |
|---|---|
| **Guarantee (Performance/Financial) :-** | |
| Guarantee Commission | 1.35% per quarter or part thereof minimum for one quarter. |
| Guarantee against 100% cash margin | 50% concession on the above rate |
| Swift Charges | **As Applicable** |
| Postages | **As Applicable** |
| Revert of Guarantee before Expiry | **Minimum 1 Qtr BG Commission to be recovered for part of quantum of full guarantee commission to be recovered** |
| Closure of Guarantee After Expiry of Claim Period | Nil |
| Invoke of Guarantee | **USD 200 or equivalent in TZS** |
| | **A. Financial Guarantees: -**<br>1. In favour of Customs/Excise/Tax Authorities towards tax/Duties payment Etc.<br>2. Favouring Courts for Release of Amounts.<br>3. For Guaranteeing Loan payments.<br>**B. Performance Guarantees: -**<br>1. In lieu of earnest money deposit<br>2. In lieu of tender deposit<br>3. In lieu of security deposit<br>4. To obtain advance payments (generally exports)<br>5. To obtain mobilization advance (generally domestic)<br>6. Towards Direct/indirect taxes to govt. in respect of specific transaction.<br>7. For Direct/indirect taxes disputes with tax Authorities.<br>8. For payment for supplies/services made /rendered<br>9. For Securing retention amount<br>10. For Bidding/tendering for Project Contacts<br>11. For Performance in terms of any agreed contact.<br>**Note: - No processing charges or documentation charges are to be levied in case of Casual BG limits issued against 100% or more cash margin.** |
| **Imports :-** | |
| LC Opening charges | 1.35% per quarter +SWIFT charges USD 75/ - |
| Against 100% cash margin | 50% concession on the above rate i.e. 0.67% per quarter +SWIFT charges USD 75/ - |
| LC Amendment Charges | Per amendment 0.40% of LC amount (minimum USD 60 and Maximum USD 325) +SWIFT charges USD 30 (Same for LC against 100% cash margin) |
| Acceptance of bills under LC | 0.60% of Bill amount Min USD 30 Maximum USD 180 |
| Retirement of bills under LC | 0.60% of Bill amount Min USD 30 Maximum USD 360 |
| Inward Bills for Collection | 0.30% of Bill amount minimum USD 150 |
| **Exports:-** | |
| Negotiation of Bills under LC | 0.60% of Bill amount Minimum USD30 Maximum USD 360 |
| Confirmation of Export LC | 0.90% per quarter +SWIFT charges USD 30/- |
| LC Advising Charges | USD 150 |
| Export Bills for Collection | 0.60% of Bill amount Minimum USD 30 Max USD 360. |
| Charges for Certifying invoices subsequent to negotiation | **USD 10 Per Invoice** |
| Clean payment Received under LC | **USD 100 per occasion** |
| Advice of transfer in transferable LC | **USD 100 per advice of transfer and acceptance commission at 0.30% Minimum USD 100** |

### OTHER DISCLOSURES (VIAMBATANISHI NYINGINEZO)

| No. | ITEM/TRANSACTION | USD | TSHS |
|---|---|---|---|
| 1.0 | **Base or Prime Lending rate** | 7.50% p.a. | 14.50% p.a. |
| 2.0 | **Maximum Spread above Base or Prime Lending rate** | 7.00% | 7.00% |
| 3.0 | **Penal interest** | | |
| a) | For Non Compliance of Terms of sanction | 3% p.a. over Regular Rate of Interest | |
| b) | For Overdrawing/ Excess Drawings due to non – payment of interest/ Instalments/ Charges | 5% p.a. over Regular Rate of Interest | |
| 4.0 | **Deposit Rate** | | |
| i) | Current Deposit | Nil | Nil |
| ii) | Savings Bank Deposit | 0.50% p.a. | 2.50% p.a. |
| iii) | Fixed/Recurring/QIC/MIC deposit | **Up to USD 10,000** | **Up to TZS 10,000,000** |
| | 6 months | 3.00% | 6.25% |
| | Over 6 months | 3.50% | 7.25% |
| | | **Over USD 10,000** | **Over TZS 10,000,000** |
| | 6 months | 3.50% | 6.75% |
| | Over 6 months | 4.00% | 7.75% |
| | * No interest is payable in case of premature withdrawal of fixed deposits | | |
| | | | |

**No Penalties & Other sanctions have been imposed by Bank of Tanzania (BOT)during the Period covered by the Disclosure**

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| | Name. | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ashish Kumar Jha | Managing Director | Signed | 15.01.2025 |
| 2. | Heriabdiel Ayoh | General Manager | Signed | 15.01.2025 |
| 3. | Robert Kibona | General Manager | Signed | 15.01.2025 |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Dk. Mpango ametoa somo kwa viongozi wa siasa na serikali

**CHAMA** Cha Mapinduzi (CCM) mwishoni mwa wiki iliyopita, kilifanya Mkutano Mkuu Maalum jijini Dodoma ambao ulikuwa na mambo mbalimbali. Mambo yaliyofanyika katika mkutano huo ni kumchagua makamu mwenyekiti Tanzania Bara kuchukua nafasi ya Abdulrahman Kinana, aliyeomba kupumzika baada ya kuwa katika nyadhifa tofauti ndani ya chama hiyo.

Jambo lingine lililowasilishwa na kujadiliwa ni taarifa za utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa kipindi cha mwaka 2022- 2024 uliofanywa na serikali ya Muungano na ile ya Mapinduzi Zanzibar. Taarifa hizo ziliwasilishwa mbele ya wajumbe wa mkutano Mkuu Maalum na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, na Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah.

Kubwa zaidi na pengine la kihistoria, ni ukomavu ulioonesha na chama hicho kwa kufanya uamuzi wa kumpitisha Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kuwa mgombea urais katika uchaguzi mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani unaotarajiwa kufanyika Oktoba, mwaka huu.

Suala hilo halikutarajiwa na baadhi ya wanachama na wajumbe wa mkutano huo kwa kuamini kwamba mchakato huo utafanyika baadaye Juni au Julai, mwaka huu, kama ilivyozoeleka. Lakini wajumbe pamoja na busara za wazee wa chama wakiongozwa na Rais Mstaafu, Dk. Jakaya Kikwete, waliona kuwa suala hilo limalizwe mapema ili kujiandaa na mipango ya kupambania chama na hatimaye kushinda uchaguzi na kuendelea kushika dola.

Pamoja na kuamua na kumpitisha Rais Samia kupeperusha bendera ya CCM katika kinyang'anyiro cha urais, chama hicho kilimteua Katibu Mkuu wake, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, kuwa mgombea mwenza katika uchaguzi huo.

Balozi Nchimbi ameteuliwa na Kamati Kuu ya CCM kuchukua nafasi hiyo baada ya Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, kumwandikia barua Rais Samia kuomba kupumzika. Katika barua hiyo kwa Rais, Dk. Mpango amesema kwa umri wake wa miaka 68 unatosha katika utumishi, hivyo anaomba kung'atuka ili kujikita zaidi na mambo yake binafsi na familia kwa ujumla.

Kwa mambo hayo yaliyofanywa na CCM yako ya kujifunza kwa vyama vya siasa na wanasiasa kwa ujumla. Miongoni mwa mambo hayo ni ukomavu wa kidemokrasia na uendeshaji wa vyama kwa misingi ya amani na utulivu.

Mambo yaliyofanywa na CCM yanaweza kuwa yameibua nongwa kwa baadhi ya wanasiasa ndani ya chama hicho ambao walikuwa na mawazo ya kuchukua fomu kupambana na Rais Samia katika uchaguzi. Uamuzi wa wengi umeheshimiwa na ndio msingi mkubwa wa demokrasia katika chama.


Pamoja na ukweli huo, kubwa zaidi la kujifunza kwa wanasiasa wa sasa na wajao ni hatua aliyochukua Dk. Mpango ya kuomba kupumzika baada ya kumalizika kwa uchaguzi mkuu. Jambo hilo ni somo kubwa kwa wanasiasa hasa wale wanaodhani kuwa wana hakimiliki ndani ya vyeo walivyo navyo, hivyo hawawezi kuondoka labda mapenzi ya Mwenyezi Mungu yatimizwe.

Hatua aliyoichukua Dk. Mpango inapaswa kuwa somo la kujifunza kwa wanasiasa kwamba wanapaswa kutumika katika nafasi kwa muda fulani kwa kufanya mambo kwa ajili ya maendeleo ya wananchi na baada ya miaka kadhaa kuamua kukaa kando kupisha watu wengine.

Wako baadhi ya wanasiasa ambao wamekuwapo katika nafasi mbalimbali za uongozi, zikiwamo za ubunge kwa robo karne au zaidi na bado hawaoneshi dalili zozote za kung'atuka. Wanasiasa hao wanapaswa kujua kwamba nafasi hizo si mali binafsi bali za utumishi kwa wananchi, hivyo wazishike kwa kitambo ili waondoke kwa heshima badala ya aibu kwa kuwa ving'ang'anizi.

Haki Dk. Mpango amechukua uamuzi ambao ni somo kubwa kwa wanasiasa na baadhi ya viongozi kwamba hakuna mtu mwenye hakimiliki ndani ya nafasi ya kisiasa au uongozi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# CHADEMA hili liwe fundisho kwenu

**KUANZIA** mwaka jana CHADEMA imekuwa kwenye mvutano mkali uliosababisha wanachama wake kugawanyika makundi mawili yanapingana vikali kwenye mitandao ya kijamii.

Makundi hayo mawili, mojawapo ni lile linalomuunga mkono Freeman Mbowe na lingine linamuunga mkono Tundu Lissu, katika kuwania nafasi ya uenyekiti taifa wa chama hicho, ambao jana walifanya uchaguzi kuamua hatima hiyo.

Tangu kuanza mchakato wa kuwania nafasi hiyo, Watanzania wameshuhudia jinsi ambavyo makundi hayo yalivyokuwa yakivua nguo chama hicho katika mikutano na waandishi wa habari.

Wakati wa uchaguzi huo wa jana, baadhi ya wanachama ambao wako upande wa vigogo hao, walifikia kuwa na 'mashindano' ya kuitisha mikutano ya waandishi wa habari kwa lengo la kuvutia upande mmoja.

Mmoja akiitisha mkutano na vyombo vya habari kulaumu upande wa mmoja wa wagombea, mwingine kesho anaitisha mkutano wa aina hiyo na kulaumu upande wa wapinzani wake ili kujiwekea mazingira ya ushindi.

Kwa mtindo huo walifikia kutoa siri za chama bila woga wakidhani wanajijenga kumbe wakiharibia chama chao, aidha kwa kujua au kwa kutojua, kitendo ambacho ni aibu kwa CHADEMA.

Kifupi ni kwamba mchakato wa kupata Mwenyekiti wa Taifa wa CHADEMA ulikumbwa na siasa za majitaka ambazo hazifai kufanywa hasa wakati huu wa kuelekea kwenye uchaguzi mkuu.

Wakati kampeni za uchaguzi mkuu zitakapoanza watakwenda kuwaambia nini Watanzania wakiwa wameshavuana nguo hadharani kwa kujionyesha jinsi walivyo ndani ya chama hicho?

Ninadhani uchaguzi wa viongozi wa taifa wa chama hicho uwe fundisho kwa wanachama na viongozi wao kwa kuzingatia kwamba kutofautiana mtazamo, maoni sio sababu ya kufikia kuumbuana kiasi hicho na kudhalilishana hadharani.

Ikumbukwe kunyamaza nako ni burasa, sidhani kuwa ni vyema mtu anapomsema mwenzake hadharani kuhusu jambo fulani ni lazima ajibiwe kwa njia kama hiyo ya kuitisha mkutano, huko ni kuendeleza siasa za jino kwa jina.

Matokeo yake siri nyingi za chama hicho zimewekwa hadharani kutokana na udhaifu wa kukosa uvumilivu. Ni muhimu kwa kiongozi yeyote kuwa mvumilivu kwa lengo la kulinda hadhi ya chama.

Huenda huo ulikuwa ni mkakati maalum wa Mbowe na Lissu wa kuweka watu wa kuwasemea kwenye vyombo vya habari ili kuvutia wajumbe wawachagu, kama ni kweli, basi mkakati huo umekiabisha chama.

Ninaamini kila chama kina changamoto zake, lakini haijawahi kutokea makada wa chama kinachojielewa wakaitisha mikutano na vyombo vya habari na kuanza kuumbuana au kupashana.

Kwa kawaida watu hujifunza kutokana na makosa, hivyo CHADEMA nao wangejifunza kutokana na mchezo wa kuumbuana na kutoa siri za chama ulifanywa wakati wa mchakato wa uchaguzi.

Jambo la msingi ni viongozi wa chama kupima athari zilizojitokeza wakati wa mikutano ya makundi hayo na kujiwekea mipango ya kuhakikisha wakati wa uchaguzi hakuna siasa za aina hiyo.

Kuwa na makundi wakati wa uchaguzi ndani ya vyama ni jambo la kawaida, lakini sio ya kufikia kuitisha mikutano ya kutoa hadharani mambo ya chama au kutoleana maneno makali.

Wenzenu wanatoleana maneno ya kuumbuana katika vikao vya ndani vya chama, kisha yanaishia huko, sio mbele ya waandishi wa habari kwa lengo la kuutangazia umma udhaifu wa chama chenu.

CHADEMA mmechafuana hadharani, katika mchakato wa uchaguzi wa ndani, mtapokelewaje na wananchi kwenye kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka huu ili wawaelewe?

Nirudie kuwa uchaguzi ndani ya chama chenu ungefaa kuwa fundisho la kuwafanya viongozi watambue makosa yaliyojitokeza hasa ya makada kutoka hadharani na kutoa siri, kitendo ambacho kinaweza kukinyima chama nguvu za kutoka hadharani na kujinadi.

HABARI KITAIFA

# Wakili kesi ya mauaji katibu wa CCM ataka upelelezi kuharakishwa

**Na Francis Godwin,** IRINGA

WAKILI upande wa utetezi, Barnabas Nyalusi katika kesi ya Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Kilolo, Christina Kibiki, ameiomba Mahakama ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Mkoa wa Iringa kuharakisha upelelezi wa kesi hiyo.

Wakili huyo alitoa ombi hilo jana mahakamani humo kwamba kesi hiyo ina mvuto mkubwa kwa jamii na wananchi wengi wanafuatilia hivyo kuomba upelelezi ufanyike haraka ili isikilizwe kwa wakati.

Upande wa Jamhuri ukiwakilishwa na mawakili Sauli Makori na Damas Sixtus, uliieleza mahakama kuwa upelelezi wa shauri hilo utakamilika ndani ya siku 90 kwa mujibu wa taratibu, nje ya hapo wataruhusu usikilizaji kuendelea.

Kesi ya Jinai namba 3404 ya mwaka 2024 ya mauaji awali ilikuwa kwa Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Iringa, Rehema Mayagilo, lakini jana ilitajwa mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Mahakama ya Wilaya ya Iringa, Adelina Ngwaya, ambaye aliahirisha shauri hilo hadi Februari 4, mwaka huu, litakapotajwa.

Waliofikishwa mahakamani hapo ni pamoja, Boniphace Ugwale ambaye ni Diwani wa Nyanzwa, Kefa Wales, Silla Kimwaga, Boniphace Ugwale Katili, Willy Chikweo na Hedikosi Kimwaga ambao kwa pamoja wanashtakiwa kwa mauaji ya Christina Kibiki.

Watuhumiwa hao wanadaiwa kutenda kosa hilo, Novemba 12, 2024 katika kijiji cha Ugwachanya, Wilaya ya Iringa.

Baada ya kesi hiyo kuahirishwa wakati waandishi wa habari wakitimiza majukumu yao ya kihabari kwa kupiga picha watuhumiwa, mmoja wa watuhumiwa, Kefa Wales alitoa vitisho kwa waandishi kwa kuwaonesha kidole cha katikati.

Hata hivyo, waandishi hao wamefikisha malalamiko yao kwa hakimu aliyekuwa akisikiliza kesi hiyo na amewashauri kuripoti vitisho hivyo polisi.

Hii si mara ya kwanza watuhumiwa hao kutoa vitisho kwa waandishi wanaoripoti kesi hiyo.

Katika viwanja vya mahakama hiyo, umati mkubwa wa wananchi wakiwamo Wana-CCM na ndugu wa marehemu Kibiki, walifika kusikiliza kesi hiyo japo idadi yao haikuwa kubwa kama awamu iliyopita.

**Hata hivyo, waandishi hao wamefikisha malalamiko yao kwa hakimu aliyekuwa akisikiliza kesi hiyo na amewashauri kuripoti vitisho hivyo polisi.**



Washtakiwa watano wa kesi ya mauaji ya aliyekuwa Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Kilolo, marehemu Christina Nindi Kibiki, wakiwa wameficha sura zao, baada ya kufikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Iringa jana, kusikiliza shtaka linalowakabili. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Serikali yaweka wazi mikakati kupata wataalamu metrolojia

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo, amesema serikali inafanya jitihada kubwa kuwa na wataalamu wengi wazalendo hivyo amewataka wanafunzi kuchangamkia fani ya metrolojia na vipimo, kwa kuwa kuna soko kubwa la ajira ndani ya nchi na Afrika Mashariki.

Alitoa ushauri huo juzi jijini Dar es Salaam alipotembelea Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) kuangalia maandalizi ya sherehe za miaka 60 tangu kuanzishwa mwaka 1965 zinazofanyika leo kwenye maeneo ya chuo hicho.

Waziri Jafo pia alikagua ujenzi wa jengo la metrolojia unaoendelea chuoni hapo ambapo litakapokamilika litachukua zaidi ya wanafunzi 4,000 kwa wakati mmoja, maabara, kumbi za mihadhara na karakana.

Alisema serikali imeamua kuwekeza Sh. bilioni 24 kujenga jengo la metrolojia na vipimo chuoni hapo kama mkakati wa kupata wataalamu wengi wa ndani wa fani mbalimbali na kuondokana na utegemezi wa wataalamu wageni.

"Naomba niwasisitize Watanzania watumie fursa ya kuwapo kwa jengo hili wachangamkie masomo haya kwasababu tunahitaji wataalamu wa ndani wengi hatutakiwi kuendelea kutegemea wa nje lazima tuzalishe wataalamu wetu wenyewe," alisema.

Pia ametembelea ujenzi wa jengo la Metrolojia Complex na kumwagiza mkandarasi kampuni ya LI JUN Construction ya China anayejenga jengo hilo kukamilisha kwa wakati na kwa ubora waliokubaliana kwenye mkataba.

Waziri Jafo alipongeza uongozi wa CBE kwa kuanzisha ujenzi huo ambao alisema utaweka mazingira wezeshi kwa wanafunzi wengi wa fani hiyo kusoma katika mazingira bora na tulivu.

"Nawashukuru wasimamizi wa kazi hii nimeona imefikia asilimia 50 na kazi inakwenda vizuri, ila mkandarasi ahakikishe azingatie ubora kwa kuhakikisha vifaa vyote vinavyotumika kama nondo vinapimwa kwenye maabara zetu na mkandarasi mshauri anayefanyakazi kwa niaba ya serikali awe makini kuona ubora unazingatiwa," alisema.

Aidha, alisema serikali imewekeza kwenye miundombinu ya elimu, ili kuhakikisha wanafunzi wengi wanapata elimu bora na yenye kuzingatia mahitaji ya ulimwengu wa sayansi na teknolojia.

Naye Mkuu wa Chuo cha CBE, Profesa Edda Lwoga, alisema jengo hilo litakaloitwa Metrology Complex litakuwa na kumbi za mihadhara, karakana na maabara na litachukua wanafunzi zaidi 4,000.

"Metrolojia ni sayansi ya vipimo na viwango na inasoko kubwa kwa watu wanaohitimu fani hiyo kwa hiyo napenda kuwahamasisha Watanzania waje wasome fani hii," alisema Profesa Lwoga.


Alisema jengo hilo litakalogharimu Sh. bilioni 24 lilianza kujengwa Mei 2023 na awamu ya kwanza inatarajiwa kukamilika mwaka 2026 na baada ya hapo itaanza awamu ya pili ya ujenzi ambayo inatarajiwa kukamilika mwaka 2029.

Mwakilishi wa Kampuni ya LI Jun Construction, Titus Kizito, alisema ujenzi unaendelea vizuri na wanatarajia kukamilisha awamu ya kwanza mwaka 2026 kama walivyokubaliana na mteja kwenye mkataba wa ujenzi huo.

"Tumechukua maagizo ya Waziri wa Viwanda na Biashara kwa uzito mkubwa sana na tutahakikisha tunazingatia ubora wa kazi kama tulivyokubaliana kwenye mkataba na jengo likamilike kwa wakati," alisema.

KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Bodi NEMC yaridhishwa utunzaji mazingira EACOP

**Na Joseph Mwendapole**

BODI ya Wakurugenzi ya NEMC imepongeza Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) unavyozingatia utunzaji na uhifadhi wa mazingira kwa kufuata matakwa yote ya Cheti cha Tathmini ya Athari kwa Mazingira.

Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Prof. Esnat Chaggu, alisema hayo jana wakati yeye na wajumbe wa bodi hiyo walipotembelea kuona maendeleo ya mradi huo katika eneo la Chongoleani mkoani Tanga.

Prof. Chaggu alisema kitendo cha kupitisha bomba chini bila kuathiri chanzo cha maji ya mto Sigi ni utaalamu wenye tija katika kuhakikisha mazingira hasa chanzo cha maji kinalindwa.

"Tulitamani kujua na kuona upitishaji wa bomba katika eneo la mto Sigi umefanyikaje lakini kwa utaalamu wanaoendelea naona hakuna tatizo lolote na bomba litapita chini ya mto na maji hayataathirika kwa namna yoyote.

"Tumeangalia pia upande wa wataalamu wanaosimamia shughuli zinazoendelea na tumefurahi kuona wataalamu wa mazingira ambao ni vijana wetu waliosoma katika vyuo vyetu na wanasimamia maendeleo ya mradi huu mkubwa na muhimu kwa Taifa," alisema Prof. Chaggu.

Akizungumza kwa niaba ya wasimamizi wa mradi huo, Mratibu wa Masuala ya Mazingira - EACOP, Joflin Bejumula, alisema mradi utaendelea kusimamia taratibu zote za utunzaji wa mazingira kama yalivyoainishwa kwenye Cheti cha Tathmini ya Athari kwa Mazingira.

"Tunaendelea kuhakikisha kwamba matakwa yote ya Cheti cha Tathmini ya Athari kwa Mazingira yanatekelezeka na kama mradi tumeweka utaratibu wa kutembelea maeneo ambayo shughuli za mradi zinaendelea na kufanya ukaguzi kubaini athari mbalimbali zinazoweza kujitokeza kutokana na shughuli tunazozifanya," alisema Bejumula.

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) litaendelea kuhakikisha kuwa miradi yote chini inatekelezwa kwa kuzingatia Utunzaji na Uhifadhi wa Mazingira kwa manufaa ya kizazi cha sasa na baadaye.




Mafundi wa umeme wakibadilisha nguzo, eneo la Posta Mpya, jijiji Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Serikali yaahidi mazingira bora kwa wafanyabiashara

**Na Elizabeth Zaya**

MKUU wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, amesema serikali imejipanga kuendelea kuimarisha mazingira bora kwa wafanyabiashara ili waweze kulipa kodi stahiki.

Mpogolo alisema hayo Dar es Salaam wakati wa Bonanza la Michezo lililoandaliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Kikodi Kariakoo, lililofanyika katika Viwanja vya Jakaya Kikwete, Ilala Dar es Salaam.

"Wafanyabiashara hongereni kwa kuendelea kulipa kodi nasi tutaendelea kuungana mkono kufanikisha jitihada hizi," alisema Mpogolo.

Mpogolo aliahidi kuendelea kushirikiana kwa ukubwa na ofisi yake, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na TRA, kuhamasisha ulipaji kodi kwa wafanyabiashara ili mkoa huo uzidi kuongoza kwa walipakodi.

Alisema katika kipindi cha uongozi wa Rais Samia Wilaya ya Ilala imepokea Sh. bilioni 305 kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo elimu, afya na barabara.

"Katika fedha hizo tumejenga madarasa, tumelipia watoto elimu msingi na sekondari, vituo vya afya, TARURA nao walikuwa wanapata kiwango kidogo cha fedha, lakini kwa kipindi hiki fedha zimeongezeka hadi kufikia bilioni 20 na hizi zote ni kutokana na ongezeko kubwa lililotokana na ukusanyaji mzuri wa kodi unaofanywa na TRA," alisema.

Mpogolo alisema kwa mwaka 2025 katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam wanatarajia kuvuka lengo kutoka Sh. bilioni 111 hadi Sh.bilioni 120 sababu ya ushirikiano mazuri kutoka kwenye kila taasisi zote za serikali.

# ACT yaanza kutia nia kwenye ubunge

**Na Halfani Chusi**

SIKU chache baada ya Chama cha ACT-Wazalendo kufungua pazia kwa wanachama wake kutangaza nia kuwania nafasi mbalimbali katika uchaguzi mkuu unaotarajia kufanyika mwishoni mwa mwaka huu, Waziri Kivuli Ofisi ya Waziri Mkuu-Bunge, Sera, Vijana Kazi na Ajira wa chama hicho, Mhandisi Petro Ndolezi, ametangaza nia ya kugombea ubunge wa Jimbo la Kigoma Kusini.

Ndolezi alitangaza nia juzi katika mkutano wa hadhara uliofanyika juzi katika Kijiji cha Nguruka Kata ya Nguruka, Kigoma.

Alisema ameshawishika kugombea nafasi hiyo kwa kile alichokiita wingi wa changamoto zinazowakabili wananchi wa maeneo hayo ambazo ana uwezo wa kuzitatua.

"Jimbo la Kigoma Kusini linakumbwa na changamoto za miundombinu ya barabara, ukosefu wa pembejeo za kilimo, migogoro ya ardhi, huduma za afya. Nitaeleza mambo mengi wakati wa kampeni nitakapopata ridhaa ya kugombea," alisema Mhandisi Ndolezi.

Alisema amekuwa mstari wa mbele kupigania agenda za vijana kupitia majukwaa mbalimbali zikiwamo za Baraza la Taifa la Vijana, kujenga uchumi wenye kuzalisha ajira nyingi, ili kupunguza changamoto ya ukosefu wa ajira kwa vijana.

Pia alisema uwapo wa mifuko ya hifadhi ya jamii jumuishi na si tu kwa wale walio katika sekta rasmi ambao kwa Tanzania ni asilimia tisa ya nguvu kazi ya Taifa na asilimia 91 hawako kwenye hifadhi ya jamii.

ACT-Wazalendo ilifungua milango kwa watiania nafasi ya urais, ubunge na udiwani kupitia Katibu Mkuu wa chama hicho, Ado Shaibu, Januari 15, mwaka huu.

Tangu pazia hilo lifunguliwe, kwa nafasi ya urais mpaka sasa waliotia nia Tanzania Bara, ni kiongozi wa chama hicho, Dorothy Semu na Zanzibar ni Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud Othman.



## KNCU yawapoza wakulima Mwika Kinyamvuo

**Na Mary Mosha,** MOSHI

CHAMA cha Msingi Mwika Kinyamvuo wilayani hapa kimepokea Sh. milioni 95 kati ya Sh. milioni 450 wanazodai Chama Kikuu cha Ushirika Kilimanjaro (KNCU) baada ya wanachama wake kukiuzia kahawa yao msimu wa mwaka 2021/22.

Akizungumza katika mkutano maalumu wa makabidhiano wa fedha hizo, Mwenyekiti wa Bodi ya KNCU, Julius Mollel, alisema hawajaja kutengua kauli ya serikali aliyotamka wanachama hao kulipwa fedha zao zote badala yake wameleta kile kilichopo.

"Wakulima wenzangu, mimi nimefika KNCU nikakuta huu mgogoro pamoja na kiasi cha fedha cha Mwika Kinyamvuo na niliagiza zisitumike hadi mgogoro utakapoisha na Waziri wa Kilimo Hussein Bashe alinikabidhi mgogoro huu kwa msisitizo mkubwa," alisema Mollel.

Alithibitisha kulikuwa na mkataba wa kuuza kahawa hiyo kwa kilo Sh. 11,250, lakini soko lilipovurugika, waliosaini walikimbia.

"Ila wakulima wakagundua tumefanya mauziano, mwekezaji akakimbia na kahawa ile ilikaa kwa muda mrefu na baadaye kuja kuuzwa na bodi ya kahawa, hivyo fedha iliyotarajiwa haikupatikana," alisema.

Alisema baada ya mauziano hayo, yalionyesha kilichoingizwa kwenye akaunti ni ya vyama vingapi na gawio la kila chama ni shingapi.

"Ndugu zangu mkataba wa milioni 400 haukufanya kazi nikisema nitawalipa milioni hizo nazitoa wapi?

Nilichouza nimekiweka wazi na waliouza ni TCB (Bodi ya Kahawa Tanzania) ni kweli nia ilikuwa njema ila biashara haikufika mwisho, kuna uzembe ulitokea na kwenye huo uzembe zipo hasara zilitokea lakini tunaendelea kuzifanyia kazi ili hasara hizo tusizibebesha wakulima pekee," alisema Mollel.

Mrajisi Msaidizi wa Mkoa wa Kilimanjaro, Jacqueline Senzighe, aliwahakikishia wakulima hao kitendo cha kupokea fedha hizo hakitengua maamuzi na kauli za serikali.

# Wanafunzi wanywa soda zilizokwisha muda wake

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

BAADHI ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Darajani na Maisaka za Halmashauri ya Mji wa Babati Mkoa wa Manyara wanadaiwa kuhatarisha maisha yao kwa kunywa soda zilizokwisha muda wake baada ya kuokota kwenye taka zilizopo kizimba cha Darajani jirani na soko la Darajani.

Madai hayo yametolewa na wakazi wa Mtaa wa Maisaka B baada ya kukumbwa na hofu ya usalama wa maisha ya wanafunzi hao kuokota soda hizo kwenye kizimba hicho.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, baadhi ya wakazi hao, walidai soda hizo ziko kwenye taka ambazo zimefurika kwenye kizimba hicho baada ya kutelekezwa kwa muda mrefu bila kuzolewa.

Mwanahamisi Ally, alidai mara ya mwisho halmashauri kuzoa taka hizo ilikuwa ni Agosti mwaka jana.

"Juzi walikuja wakazoa safari mbili basi hawajarudi sijui kuna shida gani, na huwa tunalipia fedha ya kuzoa taka kila kaya Sh. 2,500 na kwa wafanyabiashara wanatozwa Sh. 7,000 hadi Sh. 8,000 kwa mtu mmoja," alidai Mwanahamisi.

Alidai alishangazwa juzi mfanyabiashara alituma gari lenye soda hizo na kutupa kwenye kizimba hicho, ambapo waliokota na kunywa.

"Juzi kati baada ya gari kuzoa kidogo taka kuna gari limekuja limemwagа soda zilizoisha muda wake na watoto waliingia wakazikusanya wamekunywa soda hizo siku tatu mfululizo," alidai mkazi huyo wa mtaa huo.

Aliyataja madhara ambayo alidai yanaweza kusababishwa na taka hizo ambazo hazizolewi kuwa ni kutokea mlipuko wa magonjwa hasa kipindupindu na ya matumbo.

Mkazi mwingine, Doreen Mrema, alidai kuna wenzao wengine wana shida ya upumuaji na eneo hilo lina harufu kali kwa kuwa taka zinakaa zaidi ya mwezi kuondolewa.

"Hapa taka zinajaa mpaka barabarani, kiafya ni mbaya na usalama wa watoto ni mdogo," alidai Doreen

Magreth Tluway, alihadharisha kuwa taka hizo zisipozolewa kwa wakati, watoto ndio wa kwanza kupata madhara kiafya kwa kuwa wanaokota soda na vyakula.

Magreth, alisema ni bora wanaotupa taka wasichanganye na vyakula na vinywaji baridi ili kunusuru afya za wanafunzi hao na watoto wengine wa mtaani hapo.

Mwenyekiti wa Mtaa huo, Issa Mnyaruge akizungumza na Nipashe kwa simu alithibitisha madai hayo, akisema hilo eneo halifai kuwepo kizimba hicho kwa kuwa liko karibu na shule, licha ya halmashauri kulazimisha kutupa taka.

Mnyaruge, alisema uongozi wa mtaa mara kwa mara umekuwa ukialalamika kizimba hicho na kutaka kitolewe, lakini juhudi hizo zimegonga mwamba.

Alisema halmashauri hiyo inakusanya ushuru wa kuzoa taka na kupanga siku ya gari kwenda kusomba na kupeleka dampo.

"Sisi kama mtaa tulikubaliana kizimba hicho kiondolewe na muhtasari tulishapeleka kata, lakini hatuoni utekelezaji na usalama wa wanafunzi wa shule za hapo ni mdogo sana," alisema Mnyaruge.

Akizungumzia suala hilo, Ofisa Mazingira wa Halmashauri hiyo, Grace Ngoo, alisema taka hizo zitaondolewa Januari 25, mwaka huu kulingana na ratiba yao.

Kuhusu wanafunzi kunywa soda zilizoisha muda wake kutoka eneo hilo, alithibitisha kupigiwa simu na kwenda kwenye kizimba hicho.

Alisema alipofika hakukuta soda hizo na alipohoji aliambiwa walimu wameziondoa na kuziteketeza kwa kuzifungua na kumimina mtoni.

Alisema ameweka mtego wa kumnasa aliyetupa soda hizo bila kuziteketeza kwa moto kwa mujibu wa sheria ya bidhaa zilizokwisha muda wake kwa matumizi ya binadamu.



Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Prof. Esnat Chaggu (katikati), akisikiliza maelezo kutoka kwa mmoja wa wasimamizi wa mradi wa bomba la mafuta la EACOP Chongoleani, mkoani Tanga juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Watakiwa kuibua taarifa ukatili kijinsia nchini

**Na Allan Isack,** ARUSHA

RAIS Samia Suluhu Hassan amewataka wananchi kuibua na kutoa taarifa za matukio ya ukatili wa kijinsia ili serikali ichukue hatua na kutokomeza vitendo hivyo nchini.

Hayo yalisemwa jana na Makamu wake, Dk. Philip Mpango, alipomwakilisha Rais Samia kwenye ufunguzi wa Maadhimisho ya Chama cha Majaji na Mahakimu Wanawake nchini (TAWJA) yanayofanyika jijini hapa kuanzia Januari 19 hadi 23, mwaka huu.

Mpango, alisema katika kukabiliana na matukio hayo, chama hicho, kimechangia kufanya marekebisho ya sheria ikiwamo ya kuzuia na kupambana na rushwa kwa kuongeza kifungu kinachohusu rushwa ya ngono ili kudhibiti matumizi mabaya ya madaraka.

Alisema chama hicho kimeshiriki kuandaa miongozo ya majaji na mahakimu kushughulikia kesi za ukatili wa kijinsia kwa Tanzania Bara na Visiwani.

Alisema vilevile kimebadilishana uzoefu na majaji wengine duniani kwa lengo la kuongeza kasi ya kutafuta haki na usawa wa kijinsia na kutoa elimu kuhusu haki na usawa kwa wananchi.

Mpango, alisema kaulimbinu ya maadhimisho hayo kwa kutimiza miaka 25 ni "Kusherehekea utofauti na mshikamano katika usawa wa kijinsia".


"Kaulimbiu hii ni muafaka kwa kuwa inatukumbusha kazi ambazo TAWJA imefanya kuleta usawa wa kijinsia na kupinga ukatili wa kijinsia," alisema na kuongeza kuwa:

"Pia inatimizia kutambua tofauti za kijinsia zilizopo sio msingi wa kubaguana badala yake tunapaswa kutumia tofauti hizo kujenga mshikamano na usawa wa kijinsia kwa kuwa haki na usawa ujenga jamii ambayo inathamini utu wa kila binadamu bila ya kujali jinsia yake, rangi, kipato, elimu au asili."

Hata hivyo, alisema serikali imejizatiti kuimarisha usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake nchini kwa kuanzisha Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kusimamia usawa wa kijinsia.

"Serikali chini ya uongozi wa Rais Samia imeboresha utendaji katika utoaji haki ikiwamo kuhakikisha usawa wa kijinsia unakuwepo katika ngazi mbalimbali za uongozi wa mahakama na sekta nyingine," alisema Mpango.

Alisema mfumo na uendeshaji wa shughuli za mahakama umefikia hatua nzuri japokuwa bado haitoshelezi katika ukuzaji wa usawa wa kijinsia.



# Wenyeviti walilia posho 50,000/- kwa mwezi

**Na Ada Ouko,** MUSOMA

WENYEVITI wa serikali za mitaa wa Manispaa ya Musoma mkoani Mara wameiomba serikali kutenga Sh. 50,000 kuwalipa posho kila mmoja kuwasaidia kujikimu kimaisha na kulipia pango za ofisi zao.

Wenyeviti hao 73, walitoa ombi hilo juzi katika kikao chao cha kawaida cha kujadili changamoto zao katika kuimarisha utendaji wao kuwahudumia wananchi.

Mwenyekiti wa Wenyeviti hao, Aloyce Kayola, alisema kukosa fedha kunawalazimu kufanya kazi za ofisi majumbani mwao.

"Kwanza hatuna ofisi, wananchi wanatufuata kwenye nyumba zetu tuwahudumie, wanashindwa kujieleza kwa kina kwa kuwa hakuna faragha, " alisema Kayola ambaye ni mwenyekiti wa mtaa wa Mtakuja 'A' Kata ya Mwisenge na kusisitiza kuwa:

"Ikiwezekana tunaiomba serikali itulipe posho Sh. 50,000 walau kila mwezi ili ndani ya posho hiyo tuweze kupanga ofisi na kutekeleza majukumu yetu ipasavyo na wananchi kuwa huru kueleza shida zao."

Kwa upande mwingine, alisema kumekuwa na mwingiliano wa majukumu baina yao na watendaji wa kata na kuiomba serikali mkoani humo kuwapa semina elekezi kuwajengea uelewa ya mipaka kati yao na watendaji.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Kitaji 'C' Emmanuel Nguruchoni, alimwomba Mbunge wa Musoma Mjini, Vedastus Mathayo, kuwaongezea muda wa kulipia pikipiki alizowakopea kama vyanzo vya mapato katika utekelezaji wa majukumu yao.

"Tuna mapendekezo kuwa badala ya kulipia kwa miezi 11 tunaomba tuongezewe muda hadi miaka miwili kwa kuwa hatuna posho wala mishahara," alisema Nguruchoni.

Katibu wa Mbunge huyo, Seth Maendaenda, alisema ili kuwasaidia wenyeviti hao kujikwamua kiuchumi Mathayo alikubaliana na kampuni ya pikipiki kuwakopea pikipiki ili wafanyie biashara ya usafirishaji abiria 'bodaboda' na kulipia Sh. 300,000 kila mmoja na mwenyewe Sh.190,000 kama kianzio cha malipo hayo.

"Baada ya hapo mkopaji anakuwa anarejesha Sh.70 kila wiki kwa miezi 11 na anakuwa amemaliza rejesho hilo na kukabidhiwa pikipiki hiyo moja kwa moja," alisema Seth.

Katika hatua nyingine; wenyeviti hao, wamependekeza kushirikishwa kwenye vikao vya madiwani ili kupata uelewa ya thamani ya miradi wanayokabidhiwa kuisimamia.

Walidai miradi mingi inawafikia kwenye maeneo yao na kutakiwa kusimamia bila kutambua thamani yake.




Dereva wa bodaboda, akiwa ameisheheni mzigo mkubwa katika barabara ya Mwanza-Musoma, eneo la Ndama, wilayani Nyamagana jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: VITUS AUDAX**

## Polisi yanasa watuhumiwa 115 Ziwa Victoria

**Na Vitus Audax,** MWANZA

JESHI la Polisi Mkoa wa Mwanza limewakata watu 115 kwa tuhuma za uhalifu katika mialo iliyopo visiwa vya Ziwa Victoria.

Kamanda wa Polisi Mkoa huo, Wilbrod Mutafungwa, alisema kuwa watuhumiwa hao walikamatwa katika operesheni dhidi ya uhalifu iliyoanza Januari 15 hadi 20 mwaka huu mkoani hapa.

Kwa mujibu wa Mutafungwa, watu hao wanakabiliwa na tuhuma za wizi, uvuvi haramu na kuishi nchini bila kibali, kukiuka masharti ya leseni ya biashara, kucheza kamali, kujeruhi, kupatikana na pombe haramu ya gongo, bangi na kumtaja mtu mchawi.

Kamanda huyu, alisema watuhumiwa hao walikamatwa katika visiwa vya Yozu, Nyamango, Soswa na maeneo ya Kanyala na Mbugani Kata ya Bulyaheke, Halmashauri ya Buchosa baada ya jeshi hilo kupata taarifa kutoka kwa wananchi.

Mutafungwa, alisema katika operesheni hiyo, wamekamata vielelezo ikiwamo mitumbwi sita isiyokuwa na namba za usajili ambayo inatumika kufanya wizi wa mazao ya uvuvi, mashine ya kuendeshea boti, nyavu haramu 1,500 aina ya timba.

Alitaja vielelezo vingine kuwa ni kilo tano za bangi na gongo.

Alisema kati ya watuhumiwa hao, 31 wamefikishwa mahakamani, 11 kuhukumiwa kwenda jela miezi 12 baada ya kupatikana na hatia ya kufanya biashara ya ukahaba.

**Kamanda wa Polisi Mkoa huo, Wilbrod Mutafungwa, alisema kuwa watuhumiwa hao walikamatwa katika operesheni dhidi ya uhalifu iliyoanza Januari 15 hadi 20 mwaka huu mkoani hapa.**

# Soko kuu hatarini kwa magonjwa ya mlipuko

**Na Shaban Njia,** SHINYANGA

WAFANYABIASHARA na wateja wa Soko Kuu la Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga wamedai wako hatarini kukumbwa na magonjwa ya mlipuko kutokana na kupasuka kwa shimo la kuhifadhi majitaka na kusambaa kwenye maeneo yao.

Wamedai kuwa maji hayo yamesababisha harufu mbaya na uchafuzi wa mazingira hali inayohatarisha afya zao.

Wameitaka halmashauri kuboresha mazingira ya soko hilo na kuwa safi kwa kukarabati shimo hilo kulinda afya zao na wateja wao dhidi ya mlipuko wa magonjwa kutokana na uchafu.

Mfanyabiashara, Chausiku Siso, alidai maofisa wa afya hawafiki kukagua mazingira yao ya biashara na badala yake wanafika wa kukusanya mapato na ushuru bila kujali hali ya uchafu wanayokumbana nayo.

"Majitaka yanatiririka kwenye biashara zetu na maeneo mengine ya makazi ya watu waishio jirani, kama hali hii isipodhibitiwa magonjwa ya mlipuko ikiwamo kipindupindu yataibuka na kuwa tishio kwa afya zetu," alidai Siso.

Mfanyabiashara mwingine, Dafroza Girlfus, aliiomba halmashauri hiyo kujenga shimo jingine na kuwaondolea hofu ya kuzuka kwa kipindupindu na kufunga biashara zao kwa kuwa soko hilo tegemeo lao la kutafuta kipato cha familia.

Mwenyekiti wa soko hilo, William Nyahingi, alisema asilimia kubwa ya wafanyabiashara wa mboga, matunda na vyakula hawafanyi biashara kwa sababu ya maji hayo kutiririka na kusambaa kwenye eneo lao.

Mkuu wa Kitengo cha Kudhibiti Taka cha halmashauri hiyo, Kuchibanda Snatusi, alisema makaro ya vyoo vya soko hilo ni ya muda mrefu na yalikuwa kwenye mpango wa kukarabatiwa, lakini kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha, moja wapo limepasuka na kutiririsha majitaka.

Snatusi, alisema hatua za haraka zinaendelea kuchukuliwa ili kudhibiti maji hayo na magonjwa ya mlipuko kwa wafanyabiashara, wateja na wakazi wa jirani na maeneo hayo.

Alisema kazi hiyo itaanza kufanyika ndani ya wiki moja kuanzia sasa ili wafanyabiashara waendelee kufanya biashara katika mazingira ya usafi.



Ukurasa 12

**Trump anavyoanza na kukomesha vita Gaza**



Ukurasa 13

Kitete Afrika Trump anaposhika hatamu


# siasa

JUMATANO JANUARI 22, 2025

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU




Ukurasa 14

**Makamu Mwenyekiti CCM Bara, anaanzia majukumu mapya hapa**

# Upinzani wana cha kujifunza yanayofanywa na CCM

**Na Waandishi Wetu**




Viongozi wa Chadema, Freeman Mbowe (kulia) na Tundu Lissu. **PICHA: MTANDAO**

WAKATI CCM imewahi kuteua wagombea badala ya kusubiri Julai kama ilivyozoeleka kwa miaka mingi, vyama vingine hasa vya upinzani vina cha kujifunza.

CCM imeondoka Dodoma na majina ya wagombea wake wa Jamhuri ya Muungano na Zanzibar. Ni kipindi ambacho CHADEMA wanaendelea kujipanga wampe nani uongozi wa chama kati ya Mwenyekiti Freeman Mbowe na Makamu Tundu Lissu.

Jana CHADEMA walitarajiwa kuwapata viongozi wakuu wa chama kwenye uchaguzi uliofanyika jijini Dar es Salaam.

CCM imempitisha Rais Samia Suluhu Hassan, kuwa mgombea wa urais wa Jamhuri ya Muungano, wakati kwa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi amepitishwa kuwania muhula wa pili.

Baadhi ya wachambuzi wanasema ni kama kutimiza utaratibu ambao ni lazima iwe hivyo, kwa kuwa CCM ina kawaida ya kumpa mgombea urais miaka 10 ya uongozi bila kubadilishwa au kuteua mwingine kama inavyoelekezwa na katiba yake.

Kwa upande wa CHADEMA wana cha kujifunza kuwa mwaka wa uchaguzi mkuu siyo muda wa kufanya uchaguzi wa viongozi wakuu na wengine ndani ya chama badala yake wabadilishe taratibu na kuanza kujiweka kwenye kutumia mwaka wa uchaguzi mkuu kuweka na kujiimarisha na kuvuta wanachama na wapenzi wengi ili kutoa upinzani kwa chama tawala.

Mwaka 2019 Mbowe alichaguliwa tena katika nafasi ya uenyekiti dhidi ya mpinzani wake Cecil Mwambe, katika matokeo yaliyotangazwa Desemba 19, 2019.

Ukiangalia kitakachoendelea CCM ni kuwavuta na kuwaonyesha wananchi kuwa hawayumbi na kuelekea uchaguzi mkuu wako tayari ili kwa CHADEMA kinachojiri ni mnyukano wa kutafuta viongozi wa chama hicho taifa, ndipo viongozi watakaochaguliwa wajipange kwa ajili ya uchaguzi mkuu.

Inawezekana kuwa ni kuchelewa kwa upande mmoja, lakini inaweza kuwa ni kuendeleza siasa za mazoea wakati CCM wanaonyesha kubadilika.

Historia ya uteuzi wa wagombea urais ndani ya CCM inaonyesha kuwa kazi hiyo inafanyika Julai kila mwaka wa uchaguzi mkuu, lakini safari hii wamewahi na kuifanya mwanzoni mwa mwaka.

Hata hivyo, wachambuzi wanasema huenda wamejihami ili kujiepusha na upinzani ndani ya chama kama ilivyotokea 2020.

Uchaguzi mkuu wa 2020, ulishuhudia baadhi ya wana CCM akiwamo Benard Membe (marehemu) wakitangaza nia ya kugombea urais licha ya utaratibu wa chama wa kuachiana miaka 10 bila upinzani wa ndani.

Hatua hiyo ilisababisha Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki wa awamu ya tano na mbunge wa Mtama, kufukuzwa uanachama wa CCM huku ndoto yake ya kugombea urais kupitia chama hicho ikitoweshwa.

Ilikuwa ni baada ya kuhojiwa na Kamati Ndogo ya Maadili, Udhibiti na Nidhamu ya CCM mjini Dodoma ambapo pamoja na mambo mengine, alituhumiwa kwa utovu wa nidhamu, hatua zilizochukuliwa mwanzoni mwa mwaka huo.

Membe alijiunga na Chama cha ACT Wazalendo na kupewa nafasi ya kuwania urais katika uchaguzi mkuu wa mwaka huo wa 2020, huku mpinzani wake John Magufulu, akimshinda kwa kiwango kikubwa.


Pengine ni katika kuwahi kuondoa migogoro na makundi ndani ya chama, CCM ikawahi kuwathibitisha na kuwateua wagombea wake wa urais mwaka huu.


Kila masika yana mbu wake hata katika sakata hilo la Membe, baadhi ya wanachama wakongwe kama Sophia Simba, Jessica Msambatavangu na Omary Madenge walitimuliwa ndani ya chama kabla ya kurejeshewa uanachama baadaye.

Licha ya kwamba CCM imekuwa mstari wa mbele kuzuia kampeni za mapema na kutia nia ya kugombea urais. Baadhi ya wanachama walidaiwa kuonyesha nia ya kujitosa katika kinyang'anyiro.

Utauzi huo wa CCM ni kama umewapa watiania wa kificho muda wa kujitafakari na kujipanga mapema kama watakimbilia upinzani au watabaki ndani ya chama na kusubiri uchaguzi mkuu mwingine, tofauti na miaka ya nyuma walitimkia upinzani baada ya kukosa kura za kutosha katika uteuzi wa awali.


**INAENDELEA UK. 13**





Viongozi wa Hamas, Yahya Sinwar (kushoto) na Ismail Haniyeh waliouliwa na Israel mwaka jana. **PICHA: MTANDAO**

# Trump anavyoanza na kukomesha vita Gaza

**Na Christina Mwakangale**

KUSITISHWA kwa mgogoro kati ya Israel na kundi la Kipalestina la Hamas, kwenye Ukanda wa Gaza, uliodumu kwa takribani mwaka mmoja na miezi mitatu, kunakuja siku moja baada ya Rais Donald Trump, kutinga Ikulu ya White House.

Mgogoro huo umeacha athari za kiuchumi, kijamii na kiafya kwa siku 467. Shirika la Afya Duniani (WHO), linasema takribani robo ya waliojeruhiwa, watu 22,500 majeraha ni makubwa.

Kila siku watoto 10 hupoteza mguu mmoja au yote miwili. Upasuaji na ukataji wa viungo uliohitajika, ulifanyika kwa kiwango kidogo au bila ganzi.

Mazingira pia yameathiriwa na kuhatarisha afya za viumbehai, tani 85,000 za vilipuzi zilitupwa kwenye ardhi kwa miezi 15 huko Gaza.

Shirika la Umoja wa Mataifa linalowahudumia Wakimbizi wa Kipalestina (UNRWA), linasema kila siku watoto 10 hupoteza mguu mmoja au yote miwili.

Hata hivyo, upasuaji na ukataji wa viungo hufanyika kwa kiasi kidogo au bila ganzi kabisa.

Inakadiriwa tani 85,000 za vilipuzi zimetupwa huko Gaza, kulingana na Mamlaka ya Ubora wa Mazingira ya Palestina.

Marekani ni mshirika muhimu wa Israel. Utekelezaji wa makubaliano ya kusitisha mgogoro huo, unakuja baada ya Israel na Hamas, kukubali kusitisha vita huko Gaza, kwa kukubaliana kuwaachilia huru mateka wa pande hizo mbili.

> “WHO, inasema takribani robo ya waliojeruhiwa, watu 22,500, wana majeraha makubwa yaliyobadilisha maisha yao na yanahitaji ukarabati wa kiafya na hawapati.

Marekani na wapatanishi wengine akiwamo Qatar wanasema, ni kwa mujibu wa Aljazeera, yatakuwa mafanikio makubwa zaidi tangu miezi 15 ya vita, kupita.

Kundi la Wapalestina lenye silaha la Hamas liliishambulia Israel, Oktoba mwaka juzi.

Huku Trump akiingia mamlakani rasmi wiki hii, awali katika mkutano wa ushindi uliofanyika mwishoni mwa mwaka jana, mjini Washington, Marekani, alijipatia sifa kwa kuachiwa kwa mateka wa kwanza kutoka Gaza, akimpuuza mtangulizi wake Joe Biden, ambaye pia alichukua sifa kwa makubaliano hayo.

Kadhalika, Trump alitoa sifa kwa mjumbe wake mpya wa Mashariki ya Kati, Steve Witkoff.

**MATEKA WAACHIWA**

Mapema wiki hii, Israel iliwaachia huru wafungwa na mahabusi 90 wa Kipalestina. Lilikuwa ni tukio la saa chache baada ya mateka watatu wa Israel, kuachiliwa kutoka mikononi mwa Hamas huko Gaza na kurejea nchini mwao.

Kusitishwa mapigano kulianza kutekelezwa Jumapili iliyopita huku Waziri Mkuu wa Qatar, Sheikh Mohammed bin Abdul Rahman Al Thani, akisema makubaliano hayo kuanza kutekelezwa Jumapili yalipoidhinishwa ni jambo jema.

Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, anasema kuna vifungu kadhaa ambavyo havijafafanuliwa, ambavyo alikuwa ana matumaini ya kukamilishwa leo jioni.

Mkataba uliokamilika utafanya vita huko Gaza kusitishwa na kubadilishana mateka na wafungwa. Hamas iliwakamata mateka 251 ilipoishambulia Israel Oktoba, 2023.

Inawashikilia mateka 94, ingawa Israel inaamini kuwa ni 60 pekee walioko hai. Kadhalika, Israel inatarajiwa kuwaachilia wafungwa 1,000 wa Kipalestina, baadhi yao wamefungwa kwa miaka mingi, ili kuwalipa mateka hao. Kwa mujibu wa BBC.

Ikiwa usitishwaji wa mapigano utaendelea, kubadilishana kwa mateka kunatarajiwa kufanyika tena Jumamosi hii Januari 25, inaongeza BBC.

Hamas inapaswa kuwaachilia mateka wanne wa kike waliokuwa hai. Kwa malipo, Israel itawaachilia huru wafungwa 30 hadi 50 wa Kipalestina, kwa kila mateka.

**USHUHUDA WA MATEKA**

Mmoja wa mateka aliyeachiwa huru, mwanafunzi wa udaktari Mpalestina, amejumuishwa miongoni mwa wafungwa 90 walioachiwa huru na Israel. Kituo cha habari cha Aljazeera kinataarifu.

Anasema hali ya kizuizini ilikuwa mbaya na kwamba upatikanaji mdogo wa chakula pamoja na maji umezidi.

Hata hivyo, Bara'a Al-Fuqha (22), anasema alihisi ahueni na furaha kubwa kuungana tena na familia yake, huko Ukingo wa Magharibi, Jumatatu hii.

Alipokutana na familia yake, aliwakumbatia, kuwashika kutoka kwenye basi la Chama cha Msalaba Mwekundu na kuingia katika umati wa Wapalestina walishangilia, wakiwakaribisha wafungwa kadhaa, wote wanawake na watoto, waliotoka gerezani.

**CHANZO MGOGORO**

Mamia ya wapiganaji wanaoongozwa na Hamas walifanya shambulizi ambalo halijawahi kushuhudiwa kusini mwa Israel, na kuvunja uzio wa mpaka na kulenga jamii, vituo vya polisi na kambi za jeshi.

Takribani watu 1,200 waliuawa na mateka zaidi ya 250 walirejeshwa Gaza. Hamas pia ilirusha maelfu ya makombora nchini Israel.

Israel ilijibu kwa kampeni kubwa ya kijeshi, kwanza kwa ndege na kisha uvamizi wa ardhini. Tangu wakati huo, Israel imeshambulia maeneo yote ya Gaza kwa njia ya ardhini, baharini na angani, huku Hamas ikiishambulia Israel kwa roketi.

Mashambulizi ya Israel yameharibu Gaza na kusababisha uhaba mkubwa wa chakula, huku msaada ukijitahidi kuwafikia wale wanaohitaji zaidi.

**WAATHIRIWA**

Zaidi ya watu 46,700 wakiwamo watoto 18,000, wameuawa na mashabulizi ya Israel, kulingana na Wizara ya Afya ya Gaza inayodhibitiwa na Hamas.

Pia zaidi ya watu 110,265 wamejeruhiwa huko Gaza kutokana na mgogoro huo. Hii ni sawa na mtu mmoja kati ya 20.

WHO, inasema takribani robo ya waliojeruhiwa, watu 22,500, wana majeraha makubwa yaliyobadilisha maisha yao na yanahitaji ukarabati wa kiafya na hawapati.

Majeraha makali ya viungo ni aina kuu ya majeraha yanayohitaji ukarabati.

Wataalamu wanakadiria kuwa inaweza kuchukua zaidi ya muongo mmoja, kusafisha vifusi vilivyoachwa na mashambulizi hayo, ambavyo vina zaidi ya tani milioni 42, kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP).

Hatari iliyoko kwenye kazi ya kuondoa vifusi, ni kushughulikia mabomu ambayo hayajalipuka.

Karibu watu milioni 1.9 huko Gaza wamelazimika kuhama ndani ya eneo hilo, na karibu asilimia 80 wanaishi katika makazi ya muda yasiyo na mavazi ya kutosha au kinga dhidi ya baridi.

Mashirika ya Umoja wa Mataifa, yanakadiria nusu milioni wako katika maeneo yanayokumbwa na mafuriko.

Mamlaka za Gaza zimesema takriban mahema 110,000 kati ya 135,000 yanayotumika kama makazi katika Ukanda wa Gaza, yamechakaa na hayafai tena kutumika.

# Kitete Afrika Trump anaposhika hatamu

## • Hofu kutosa AGOA, Lobito

**Na Waandishi Wetu**

DONALD Trump amekula kiapo na sasa ni Rais na Amiri Jeshi Mkuu wa Jeshi la Marekani kwa awamu ya pili.

Wakati anaingia White House Afrika inajitafuta kufahamu hatima yake wakihofia itakuwaje? Utawala huo mpya wa Trump utakuwa na manufaa kwa bara lao?

Itakumbukwa kuwa wakati wa uongozi wake wa awamu ya kwanza anadaiwa kuwa aliipuuza Afrika na kuna wakati alisema Afrika ni wavivu, wasiojituma na kwamba itapendeza kama watatawaliwa tena kwa miongo mingine na kuongeza kuwa ni 'shithole'

'Shithole' si shimo la kinyesi kama ambavyo Watanzania wengi wangetafsiri, maana halisi ni kwamba ni kitu kilicho katika hali mbaya, kibovu, kilichokosa matunzo kilicho taabani kwa ubovu na kukosa uangalizi.

Rais Trump hakufanya ajizi, aliupunguza baadhi ya fedha za miradi ya ufadhili, kuwazuia na kuwakomesha wahamiaji kuingia Amerika na kulaumu kuwa wanapaswa kujitahidi kujiletea maendeleo.

Kwa ujumla Trump anachosema ni kuitaka Afrika iamke na kuachana na 'uombaomba' lakini pia ikitumia vibaya fedha za maendeleo inayopewa. Afrika ina karibu wastani wa miongo sita ya uhuru lakini kwingo cha maendeleo ni kidogo mno licha ya kuelemewa na deni kubwa kutokana na mikopo iliyochukuliwa kwenye taasisi za fedha, hazina za nchi mbalimbali na hata mashirika ya maendeleo.

Kama ilivyokuwa kwa utawala wa Joseph Biden, wa Democrat Marekani ambaye aliiweka Afrika kuwa kwenye washirika muhimu wa Marekani, Trump kipaumbele chake ni 'Amerika kwanza' au Make 'America Great Again'.

Kwa mujibu wa BBC mwaka 2023, Marekani ilieleza kuwekeza zaidi ya Dola bilioni 22 (Sh. Trilioni 55.3) tangu Biden aingie madarakani na kwamba kuna wasiwasi kuwa Trump anaweza kuondoa uwekezaji na biashara hiyo.

Rais wa hivi karibuni ana



Rais Trump wa Marekani. **PICHA: MTANDAO**

mtazamo wa kulinda zaidi maslahi ya nchi yake, usio wa kawaida kuliko Biden moja ya kauli mbiu za muhula wake wa kwanza ilikuwa "Amerika Kwanza".

Mkataba wa Ukuaji na Fursa ya Affika (AGOA), ambao umewezesha nchi za Affika kuuza nje baadhi ya mazao yao kwenda Marekani bila kulipa kodi tangu mwaka 2000, ni chanzo kikuu cha wasiwasi kuwa kitaondoka.

Mkataba wa AGOA, utawala wa Trump hakuupenda alisema hautaongezwa muda wakati utakapoisha mwaka huu 2025.

Na wakati wa kampeni yake mwaka jana aliahidi kuongeza ushuru wa mapato wa asilimia 10 kwa bidhaa zote zinazotoka nje. Hii itafanya bidhaa zikiwamo za AGOA kutozwa ushuru na kuwa ghali zaidi, na hivyo wafanyabiashara wa Afrika watakuwa wamefungiwa nje kuuza kwenye soko kubwa la Marekani. Yote hayo yataiathiri Afrika.

### UKANDA WA LOBITO

Mradi wa Lobito Corridor, ni uwekezaji mkubwa wa miundombinu wa nchi za Afrika na Marekani ambazo ni Marekani, Angola, DRC na Zambia na Tanzania kwa upande mwingine.

Ndicho kitu kikubwa ambacho Marekani ya Biden ilidhamiria kuuendeleza. Sehemu muhimu ya mradi huo ni kuunganisha huduma ya reli kati ya nchi hizo tatu na Bandari ya Lobito iliyoko Angola kwenye ufukwe wa Bahari ya Atlantic Angola.

Lengo la mradi huo umekuwa sehemu kuu ya Sera ya Ushirikiano ya Marekani na Afrika katika miaka ya hivi karibuni.

Lobito Coridor inatarajiwa kuenea hadi Tanzania katika siku zijazo ili kuunganisha Bandari ya Dar es Salaam na ya Lobito. Mpango huo unahusisha kusahihisha njia za reli zilizopo na kujenga kilomita 800 za njia mpya, hasa nchini Zambia.

Malengo ya Lobito ni pamoja na kukuza maendeleo ya uchumi wa ndani na ushirikiano wa kiuchumi wa kikanda lakini kubwa zaidi ni Marekani kupata madini muhimu ya kimkakati (critical minerals) yanayohitajika sasa kutengeneza bidhaa za kielektroniki na kufanikisha maendeleo ya teknolojia ya kidijitali na kulinda mazingira.

Kwa umuhimu zaidi Marekani inataka kubadilisha mnyororo wake muhimu ya kupata madini hayo na kuachana na utegemezi wa China ili kujipatia shaba, kobalt, nikeli na madini mengine muhimu kwa uchumi wa Marekani na msingi wa mali ghafi za viwanda vya usalama na ulinzi vya nchi hiyo.

### MADINI YA KIMKAKATI

Madini muhimu au ya kimkakati ni shaba, lithiamu, nikeli, kobalti na Rare Earth Elements ambao ni mchango wa madini mbalimbali. Madini hayo ni muhimu katika teknolojia nyingi za kielektroniki na kwenye kuunda mitambo ya kuzalisha nishati safi. Madini hayo hutengeneza 'paneli' za umeme jua na upepo, simu, ndege hadi betrii za magari ya umeme.

### CHA KUTAFAKARI

Kwa ujumla kusaidia miundombinu ya Afrika kama reli na barabara haijawahi kuwa kipaumbele cha Marekani licha ya kwamba Shirika la Changamoto za Milenia (MCA) limefadhili miradi ya barabara na umeme lakini kwa Lobito ndiyo mara ya kwanza kuanzisha ushiriki mkubwa zaidi wa miundombinu barani Afrika, Trump akiuzima itakuwa jambo la kuhuzunisha.

Sio tu mradi wa reli ni zaidi kwa sababu unahusisha kuunganisha nchi za Ushirikiano wa Maendeleo Kusini Mwa Afrika (SADC) kidijitali, kuongeza urahisi wa usafirishaji wa watu na shehena, kujenga viwanda na kuongeza ajira kwa vijana hasa kwenye kuchimba madini ya kimkakati na kuchochea ukuaji wa uchumi wa ukanda huo, kuendeleza kilimo, ufugaji na kuimarisha mnyororo wa thamani.

Ni wazi kuwa kuboresha reli kunahitajika nchini DRC, Angola, Zambia na Tanzania.

BBC inasema kuwa ingawa Trump hakutaka AGOA, na tena ameahidi kuongeza kodi bidhaa za kigeni anakabiliana na ushawishi wa kiuchumi wa China, Afrika, ambao ni mkubwa hivyo analazimika kudumisha ushirikiano.

Mwaka 2018 utawala wa Trump ulizindua Prosper Africa mpango ambao unaowezesha kampuni za Marekani zinazotaka kuwekeza Afrika na Shirika la Fedha la Maendeleo (DFC), ambalo linafadhili miradi ya maendeleo Afrika na duniani kote.

Biden aliendelea kuendesha baada ya kuchukua wadhifa wake na DFC inasema hadi sasa imewekeza zaidi ya Dola bilioni 22 (Sh. Trilion 55.3). Ikizingatiwa kuwa China bado ina nguvu kubwa barani Afrika na kwamba Trump alianzisha sera hizo mwenyewe, kuna uwezekano mkubwa wa kutafakari zaidi kabla ya kuziondoa.

# Upinzani wana cha kujifunza yanayofanywa na CCM

**INATOKA UK. 11**

Wapo baadhi ya makada kama Waziri Mkuu mstaafu Edward Lowassa (marehemu), ambaye alihamia CHADEMA mwaka 2015 na kupewa nafasi ya kuwania urais, kadhalika Membe naye baada ya kufukuzwa CCM.

Uteuzi huo wa Dodoma uwe king'ora cha kuiamsha CHADEMA na upinzani kwa ujumla kuwa hakuna wakati wa kupoteza kama wanataka kuingia katika uchaguzi mkuu na kushindana bila kuwa na 'figisu.'

Lakini pia vyama vya siasa visiishi kwa kukariri muda na matukio, bali linalowezekana leo lisingoje kesho, hasa masuala yanayohusu uchaguzi kwa ujumla.

Vyama vya upinzani vingejifunza namna bora ya kukabiliana na makundi yanayoongeza mgawanyiko katika vyama na kusababisha vikose nguvu ya kuikabili CCM.

La muhimu zaidi wakati huu ni kuwaunga mkono na kuwapa nguvu wagombea wanaokubalika badala ya kila chama cha upinzani kusimamisha mwanachama wake hata kama hafahamiki.

Si vibaya kujifunza kwa chama kinachoonekana kufanya vizuri kwa ajili ya maendeleo na ustawi wa demokrasia, ikiwamo kuiga yale ambayo yamefanywa na ACT Wazalendo na CCM.

### UTEUZI WA NCHIMBI

Mkutano Mkuu Maalum wa CCM, umeandika historia baada ya kumteua mgombea mwenza urais, Dk. Emmanuel Nchimbi ambaye atamrithi Dk. Philip Mpango, baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Dk. Nchimbi anaonekana kuwa mpole, mnyenyekevu na msikivu asiye na siasa za majitaka anayejali na kuwa kiungo muhimu katika kufanikisha mustakabali wa R4 za Rais Samia.

Mwanasiasa huyo mwenye msimamo usioyumba, wakati wa mchakato wa uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka jana, baada ya kusajiliwa mapingamizi mengi dhidi ya wapinzani, aliomba Ofisi ya Rais -TAMISEMI kuangalia uwezekano wa kuachana na mapingamizi yasiyo na mashiko ili kupiga kura na kupanua demokrasia.

Kadhalika, Nchimbi ambaye ni mwanadiplomasia, sio mtu mwenye papara, kiburi cha uzima wala si mfuasi wa siasa za jino kwa jino au ukipigwa ni lazima urudishie.

Ana imani kwamba upinzani si uadui kama ambavyo Rais Samia amekuwa akisema wapinzani ni sehemu ya Watanzania na washauri ikiwataka wakosoe serikali kwa hoja na kupendekeza ufumbuzi wa hoja zao ili kuleta maendeleo.

Dk. Nchimbi anaweza kuchukuliwa kama kiunganishi cha CCM, vyama vya upinzani, serikali na wananchi, pale ambapo kuna jambo haliko sawa anaweza kulisawazisha.

WASIRA NDANI YA NYUMBA

# Makamu Mwenyekiti CCM Bara, anaanzia majukumu mapya hapa




Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan akiongoza Kikao cha Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC), jijini Dodoma. Kushoto ni Makamu Mwenyekiti wa CCM Visiwani na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi na kulia ni Katibu Mkuu wa CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi. **PICHA: IKULU**

**Na Sabato Kasika**

SIKU chache baada ya kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Stephen Wasira anazungumza na Nipashe na kutangaza kile anachokilenga kuwa ni jukumu la kutangaza utekelezaji wa ilani ya uchaguzi mkuu wa chama chake ya mwaka 2020.

Anataja sababu ya kufanya hivyo kuwa ni kutaka wananchi wajue maendeleo yaliyoletwa na serikali ya CCM, katika kipindi cha miaka mitano ili chama kichaguliwe tena uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

"CCM imetekeleza ilani yake kwa kujenga zahanati, vituo vya afya, hospitali, shule, miradi ya maji na mingine mingi ya maendeleo, hivyo ni vyema niende kwa wananchi kuwaelezea hayo," anasema Wasira.

Mwanasiasa huyo mkongwe anasema suala la kushika dola linahitaji kuwatekelezea wananchi kile ambacho umeahidi ili wakuchugue tena, na kwamba CCM imetekeleza ilani yake.

Wasira anasema ni wajibu wa CCM kuwaonyesha wananchi kile ambacho waliahidi kuwafanyia, kwa kuwa kushika dola kunatokana na ridhaa yao hasa pale ahadi za kuwaletea maendeleo zinapotimizwa.

"Lakini kwa manufaa ya Watanzania wanaotaka kunifahamu vizuri, ni vyema niwaelezee jinsi ambavyo nimekuwa ndani ya chama na serikali na utendaji kazi wangu uliotukuka," anasema.

Anasema mwaka 1970, kwa mara ya kwanza alichaguliwa kuwa mbunge akiwa na umri wa miaka 25 katika Jimbo la Mwibara, Wilaya ya Bunda, wakati huo akitokea Wilaya ya Geita alikokuwa akifanya kazi kama Katibu Mtendaji wa TANU Wilaya.

> "Kabla ya kuwa Katibu Mtendaji wa TANU wa wilaya, nilianza kazi katika Idara ya Maendeleo ya Jamii wilayani Ukerewe mkoani Mwanza kwenye Kijiji cha Mriti.



Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Stephen Wasira (kulia), akipokea Ilani ya Uchaguzi ya CCM kutoka kwa Katibu Mkuu wa chama hicho, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi. **PICHA: MAKTABA**

Wakati huo Sengerema na Nyangh'wale zilikuwa ndani ya wilaya ya Geita, lakini sasa nazo ni wilaya tena Geita ni mkoa.

"Kabla ya kuwa Katibu Mtendaji wa TANU wa wilaya, nilianza kazi katika Idara ya Maendeleo ya Jamii wilayani Ukerewe mkoani Mwanza kwenye Kijiji cha Mriti," anakumbusha.

**MBUNGE 'MCHANGA'**

Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, anasema mwaka 1970 akiwa na miaka 25, alichaguliwa kuwa mbunge wa Jimbo la Mwibara wilayani Bunda mkoani Mara, akiwa na umri mdogo, kisha ilipofika 1975 akateuliwa kuwa Naibu Waziri wa Kilimo.

"Mwaka huo wa 1975 niliteuliwa kuwa mkuu wa mkoa wa Mara nikiwa na umri wa miaka 30. Ilipofika 1982 hadi 1985 nilikwenda kufanya kazi katika ubalozi wa Tanzania huko Washington DC, nikapata fursa ya kusoma vyuo vikuu nikigharamiwa na Mwalimu Julius Nyerere 1985 nilichaguliwa kuwa mbunge wa Bunda," anasema.

Mkongwe huyo anafafanua kuwa mwaka 1987 Rais wa Awamu ya Pili, Ali Hassan Mwinyi alimteua kuwa Naibu Waziri wa Serikali za Mitaa na Vyama vya Ushirika, Mwaka 1989 hadi 1990 alikuwa Waziri Kamili wa Kilimo na Mifugo.

"Mwaka 1990 hadi 1991 niliteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Pwani, wakati nikifanya kazi hiyo ya ukuu wa mkoa huko Mara na Pwani, vilevile nilikuwa katibu wa chama cha TANU au CCM," anasema.

Anaongeza kuwa ni mzoefu ndani ya chama na serikali, na kwamba mwaka 2005 hadi 2015 ilikuwa ndani ya serikali ya awamu ya nne, na kwamba kila Baraza la Mawaziri lilipobadilishwa, bado aliniteuliwa.

"Kuwa katika serikali za awamu karibu zote, kumenipa uzoefu mkubwa wa masuala ya kitaifa na kimataifa, kufanya shughuli za serikali na chama kumeniwezesha kuijua vyema nchi yetu. Mimi ni miongoni mwa Watanzania wachache wanaoijua Tanzania ya jana ya leo na wanaozungumza Tanzania ya kesho," anasema.

**WASIRA NI WA NANE**

CCM imempata Makamu Mwenyekiti Taifa wa nane tangu chama hicho kilipoanzishwa mwaka 1977 baada ya kuunganishwa na Chama cha Afro Shirazi Party (ASP) cha Zanzibar.

Wasira anachaguliwa na wajumbe wa Mkutano Mkuu Maalum wa CCM Taifa jijini Dodoma wiki iliyopita ili kuziba nafasi hiyo ilioachwa na mtangulizi wake Abdulrahman Kinana.

Kabla ya Wasira, wapo makada wa CCM waliowahi kushika nafasi hiyo wa kwanza ni Aboud Jumbe Mwinyi, aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa CCM kuanzia mwaka 1977 hadi 1984.

Baadaye nafasi hiyo ilishikiliwa na Ali Hassan Mwinyi, kuanzia mwaka 1984 hadi 1990 kisha akafuata Rashid Kawawa aliyeongoza kuanzia 1990 hadi 1992. Viongozi wote hao ni marehemu.

John Malecela alifuatia akashika nafasi hiyo kuanzia 1992 hadi 2007 akamwachia Pius Msekwa mwaka 2007 hadi 2012 kisha ikawa ni zamu ya Philip Mangula 2012 hadi 2022.

Mangula aliandika barua ya kujiuzulu nafasi hiyo akielezea kuwa ana sababu binafsi ndipo nafasi yake ikachukuliwa na Kinana ambaye mwaka jana aliandika barua ya kujiuzulu nafasi hiyo.

Baada ya Kinana kijiuzulu, wajumbe wamemchagua Wasira kuwa Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara ambaye amaweka wazi jukumu alilonalo wakati huu wa kuelekea kwenye uchaguzi mkuu.



## Tume ya Sefue, walipakodi uso kwa uso

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MWENYEKITI wa Tume ya Rais ya Maboresho ya Kodi, Balozi Ombeni Sefue amewahimiza walipakodi nchini kutoa maoni yao ili kuboresha mfumo wa kodi na kuondoa changamoto zinazowakabili.

Balozi Sefue alitoa kauli hiyo juzi jijini hapa wakati akijibu malalamiko ya walipakodi yakilenga kupunguza utitiri wa kodi, kupanua wigo wa mlipakodi, watendaji wa mitaa kupewa elimu ya kutosha ya kodi na kuipeleka kwa wananchi na maofisa kodi kuwa na weredi kutekeleza majukumu yao.

Malalamiko hayo yaliwasilishwa katika kikao cha pamoja cha tume hiyo, walipakodi na wadau wengine mkoani hapa kwa lengo la kupokea maoni kuhusu kuboreshwa kwa mfumo huo na kupata mwarobaini wa kudumu wa kutatua changamoto hizo.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameyasikia malalamiko mengi yakiwamo hayo na kuamua kuunda tume hiyo kisha kurejea kwa wananchi hususani walipakodi kukusanya maoni na kuyawasilisha kwake kufanyiwa kazi.

"Rais ameyasikia malalamiko mengi kutoka kwenu walipakodi ndio maana Tume tumerejea kupata maoni yenu ili yaende kufanyiwa kazi kwa ajili ya kuondoa changamoto mnazokutana nazo kupitia mfumo huo wa walipakodi," alisema Balozi Sefue.

Alisema wamelazimika kupokea maoni kuhusu namna ya kuboresha mfumo wa kodi kwa sababu tume yao haiwezi kuandika bila kuwasikikiza walipakodi nchini.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mjini, Jabir Shekimweri alipendekeza kuwapo namna ya mahususi ya kikodi ambayo itawawezesha kuwaandaa wafanyabiashara wadogo kushiriki katika uchumi shindani kupitia ulipaji kodi.

Shekimweri, alisema tume hiyo ikifanywa hivyo, itatoa mwamko kwa wafanyabiashara wadogo kushiriki kulipa kodi na kuongezekwa kwa pato la taifa na ubunifu wa biashara zao.

"Tunaomba hilo Mamlaka ya Mapato Nchini (TRA), iliangalie kwa ukaribu, ikiwezekana watanue wigo wa utendaji kazi zao ili wawe karibu na walipakodi," alisisitiza mkuu huyo wa wilaya.

Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa huo, Mwajabu Nyamkomora, alisema Rais Samia kaunda tume hiyo ili kusikiliza changamoto ya walipakodi kwa sababu kundi hilo lina mchango mkubwa kwenye kukuza uchumi wa nchi na pato la taifa.

Mwajabu, aliitaka tume hiyo kujenga mazingira ya kuwezesha biashara za wafanyabiashara hayo kuimarika na kuongeza kipato chao na familia zao.

# Wanaume vinara malalamiko Kampeni ya Mama Samia

**Na Ibrahim Joseph,**
DODOMA

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, amesema wanaume wanaongoza kwa kujitokeza kutoa malalamiko kwenye Kampeni ya Huduma ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia.

Dk. Ndumbaro alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari uliofanyika ofisini kwake katika Mji wa Serikali Mtumba jijini hapa.

Alisema wananchi 775,119 wamehudumiwa kupitia kampeni hiyo katika mikoa 11 nchini huku wanaume wakiongoza kwa kujitokeza kutoa kero na malalamiko yao kupitia kampeni hiyo.

"Haya ni mafanikio makubwa kutokana na kuwasaidia wanaume kufikisha kero zao. Nawaomba na wengine kuendelea kujitokeza kutoa kero zao kwa sababu ni siri ya mhusika na mtoa huduma wa kampeni," alisema Ndumbaro.

Alibainisha kuwa katika idadi hiyo ya wananchi waliohudumiwa na kampeni hiyo wanawake waliojitokeza ni asilimia 49 na wanaume ni asilimia 51.

Alisema wanaume wameonyesha mwitikio mkubwa wa kujitokeza na kutoa kero zao na kuondoa dhana iliyojengeka kuwa wamekuwa wakijificha hata wakinyanyasika.

Aliongeza kuwa kampeni hiyo imepunguza mashauri mahakamani kutokana na kutatua migogoro iliyopo kwenye jamii.

Aliitaja mikoa hiyo 11 kuwa ni Morogoro, Manyara, Singida, Mara, Simiyu, Ruvuma, Shinyanga, Iringa, Songwe, Dodoma na Njombe.

Kwa mujibu wa waziri huyo, kampeni hiyo itaendelea kwenye mikoa mingine sita lengo ni kuhakikisha inaifikia mikoa yote nchini kabla ya Machi mwaka huu.

Aliitaja mikoa ambayo kampeni itaanza Januari 24, mwaka huu kuwa ni Tabora, Kigoma, Geita, Kilimanjaro, Mtwara na Katavi.

Ndumbaro, alisema kampeni hiyo itafanyika kwa siku tisa na kuwafikia wananchi waliopo maeneo ya vijijini na mijini kwa kushirikiana na watoa huduma kutoka Chama cha WanasheriaTanganyika (TLS) na wengine wa sheria.



Sheikh Mkuu wa Tanzania, Mufti Dk. Abubakar Zuberi, akimwagilia maji mti baada ya kuupanda katika eneo la Msikiti wa Gaddafi, jijini Dodoma jana, baada ya kufanya ziara ya kukagua miradi ya uwekezaji inayomilikiwa na Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA). **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Michango kujiunga sekondari ilivyomshtua RC Dendego

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, ameshtushwa na fomu ya mwanafunzi kujiunga na kidato cha kwanza kuwa mzigo kwa wazazi na walezi na kutoa siku saba kwa Idara ya Elimu kutengeneza moja inayofafana na kutumika kwa mkoa mzima ili kudhibiti michango holela na kero kwao.

Amri hiyo aliitoa kwenye Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) Dendego, alisema utaratibu wa kila sekondari kuwa na fomu yake ya kujiunga na sekondari unasababisha mzigo mkubwa kwa wazazi kutokana na kila mwanafunzi kuagizwa vitu vingi kuwa navyo anapoonza masomo.

"Mtoto mmoja anaambiwa kalete jembe, fyekeo, panga na vingine, nimesoma fomu moja ni hatari mtoto anaagizwa kupeleka vitu vingi sana kwa hiyo tukubaliane tuwe na fomu moja na kama tunahitaji michango ya ziada tumekubaliana namna ya kuomba hiyo michango lakini ni lazima wazazi waridhie," alisema.

Dendego alisema utitiri wa michango unaondoa maana halisi ya elimu bure kwa wanafunzi na kwamba katika Mkoa wa Singida ni marufuku michango holela inayowaumiza wazazi.

"Hivyo vitu mnavyowaagiza wanafunzi mnavipeleka wapi sio sawa 'it is too much', nyie mnaweza kuona mpo hapa mjini maisha ni mepesi, lakini vijijini ni mzigo mkubwa tunawapa wazazi matokeo yake ndio maana watoto hawaji shule," alisema.

Vilevile, alipiga marufuku mwanafunzi kufukuzwa shule kwa sababu hajapeleka jembe, panga, fyekeo na ambaye hana sare.

Katika hatua nyingine, alishushua Idara hiyo ya Elimu kwa kusema inadanganya kuhusu takwimu kuwa asilimia 100 ya shule za sekondari katika mkoa huu zinatoa huduma ya chakula kwa wanafunzi.

"Hizi takwimu hapa mnanidanganya, mimi nimefanya ziara maeneo mbalimbali wanaopata chakula ni wanafunzi wa madarasa ya mitihani tu na sio wanafunzi wote," alisema.

Awali Kaimu Ofisa Elimu Mkoa huo, Imani Mwaipaja, alisema hadi kufikia Desemba mwaka jana, hali ya utoaji wa chakula kwa wanafunzi wa sekondari ni asilimia 100 kwa shule zote 194.

Mwaipaja, alisema kwa upande wa shule za msingi 691 hali ya utoaji huduma ya chakula kwa wanafunzi imefikia asilimia 95 kwa kipindi hicho.





# Kiwanda kuanza kuchakata parachichi mwezi ujao

**NA Elizabeth John,**
NJOMBE

KIWANDA cha kuchakata parachichi kwa ajili ya kutengeneza mafuta kinachojengwa katika Halmashauri ya Mji wa Makambako mkoani Njombe kinatarajia kuanza kufanya kazi Februari mwaka huu.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Avo Africa, Najib Kamal, alieleza hayo juzi wakati akitoa taarifa ya kiwanda hicho kwa Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka ambaye alifanya ziara ya kukagua kiwanda hicho.

Alisema kiwanda hicho mpaka kukamilika kwake kinatarajia kugharimu Sh. bilioni 20 na gharama hizo ni kwa ajili ya mashine na vifaa vingine vitakavyokuwapo katika kiwanda hicho cha kuchakata mafuta.

Alisema kiwanda hicho kina mashine mbili na kitakuwa na uwezo wa kuchakata tani 600 za parachichi kwa siku na ifikapo Juni mwaka huu wataongeza mashine zingine mbili, hivyo kuwa na uwezo wa kuzalisha tani 1,200 kwa siku.

"Huu ni mradi wetu wa pili wa kwanza ni ule wa kupaki parachichi na kusafirisha nje ya nchi lakini wa pili ni huu wa kuzalisha mafuta yanayotokana na parachichi na tunatarajia kuwa wazalishaji wakubwa wa mafuta hapa nchini," alisema Kamal.

Alisema kiwanda hicho kitakapokamilika kitakuwa na uwezo wa kuajiri wafanyakazi wasiopungua 400 hii inajumuisha wataalamu pamoja na wale watakaokuwa wanakwenda shambani kwa ajili ya kufuata bidhaa hiyo.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, alisema ujenzi wa kiwanda hicho ni mkombozi mkubwa kwa wakulima wa parachichi mkoani humo kwani tofauti na ilivyokuwa awali mkulima alikuwa anauza kwa bei ndogo kutokana na hofu ya tunda kuharibika lakini sasa atakuwa na maamuzi ya bei.

Hata hivyo, Mtaka alimpongeza mkurugenzi wa kiwanda wa Najib Kamal kwa kuitikia kauli mbiu ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuwatoa hofu wawekezaji ambao wana nia ya kuwekeza hapa nchini kuwataka kufanya hivyo na serikali itawaunga mkono.

Kwa upande wake, Ofisa Kilimo Mkoa wa Njombe, Wilson Joel alisema makadirio ya parachichi ambazo zilikuwa zinakataliwa kutokana na kukosa ubora kwa mkoa wote ni tani 20,000, hivyo kama kiwandani kitauchukua zaidi ya tani 10,000 maana yake zaidi ya asilimia 70 ya parachichi hizo zitachukuliwa na kiwanda hicho.

"Nafikiri itakuwa mchango mkubwa sana kwenye sekta sisi tutaendelea kushirikiana na wewe ili kuweza kuwafikia wakulima ili hizo parachichi zikufikie," alisema Joel.

Msimamizi wa ujenzi wa kiwanda hicho kutoka kampuni ya Amenduni iliyopo Italia, Victor Mutua alisema mashine za kiwanda hicho zitakuwa na uwezo wa kuzalisha tani 600 kwa muda wa saa 12.



Katibu Tawala wa Mkoa wa Iringa, Doris Kalasa, akizungumza wakati wa kusikiliza changamoto mbalimbali za walimu, mjini Iringa juzi, kupitia timu ya Samia Teacher Mobile Clinic. Kushoto ni Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Suleiman Komba na Mwenyekiti wa CWT Iringa, Gaur Mgalula (kulia). **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Makete yapewa tani 240 ya mbegu za ngano

**Na Elizabeth John,**
MAKETE

SERIKALI imetoa tani 240 ya ruzuku ya mbegu za ngano wilayani Makete mkoani Njombe ikiwa ni awamu ya kwanza ya utolewaji wa mbegu hizo kwa msimu mpya wa kilimo mwaka 2025/2026.

Akizungumza juzi baada ya kupokea mbegu hizo, Mkuu wa Wilaya ya Makete, Juma Sweda alisema wamepokea mbegu hizo ili wananchi walime na kuisaidia serikali kupunguza uagizaji wa mbegu hizo kwenye mataifa mengine.

"Tumeshapokea tani 240 za mbegu ya ngano, kwa msimu huu ikiwa ni tayari kwa ajili ya msimu huu mpya wa kilimo, hii ni awamu ya tatu ya utolewaji wa mbegu hizi kwasababu tumeshapokea kwa awamu mbili huko nyuma na hii yote ni kwamba serikali ipo makini na inataka kupunguza uagizaji wa ngano nje ya nchi," alisema Sweda.

Sweda aliwataka wakulima wa Wilaya ya Makete kuhakikisha kuwa wanachangamkia fursa hiyo kwa kuanza kulima mapema ili waendane na hali ya hewa ya ukanda huo.

Kwa upande wake Mratibu wa ngano Wilaya ya Makete, Ahmed Kichombaki, alisema kuwa wametenga sehemu tatu za upokeaji na ugawaji wa mbegu hizo za ruzuku.

"Sehemu hizo ni eneo la Soko la Ngiu lililopo Kata ta Iwawa, Tandala pamoja na Mfumbi, kulingana na uhitaji wa wakulima na lengo ni kupokea tani zaidi ya 1,000 za mbegu hii kutokana na mahitaji makubwa ya wakulima na kuwapo kwa mashamba ya kutosha pamoja na mwamko mkubwa wa uhitaji wa mbegu hizi," alisema Kichombaki.

Kichombaki aliongeza kuwa mbegu hizo zimekuwa zikiuzwa Sh. 4,000 kwa kilo, hivyo mkulima kama angetaka kuwekeza katika kilimo hicho ingekuwa ikimlazimu kutumia Sh. 280,000 kwa kila eka, ili aweze kupata mbegu hizo kulingana na uhitaji.

Mmoja wa wakulima wa ngano Wilaya ya Makete, Jeita Mahenge alisema kuwa soko la zao hilo limekuwa kubwa kutokana na kampuni kubwa kuingia moja kwa moja kwa wakulima kununua zao hilo, sambamba na wao wenyewe kuzalisha baadhi ya vyakula kama vile mikate pamoja na unga.

# Wafanya maombi kuita mvua, kuondoa ukame

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANANCHI wa Kata ya Utengule Halmashauri ya Mji wa Makambako wilayani Njombe wamefanya maombi ya kuomba mvua ili kukabiliana na hali ya ukame ambayo imesababisha baadhi yao washindwe kulima kwa wakati na mazao kukauka.

Wakizungumza na Nipashe baada ya maombi ambayo yaliyofanyika katika Kijiji cha Ikelu Makambako, wananchi hao walisema katika kijiji chao miaka yote wamezoea shughuli za kilimo hasa kulima na kupanda huwa zinaishia Desemba lakini kwa msimu huu imekuwa tofauti kwani mpaka sasa bado wanalima na kupanda mahindi.

Mmoja wa wananchi hao akiwamo, Monica Msalilwa alisema wamelazimika kufanya maombi ya kumwomba Mungu kuwaletea mvua ambayo itawasaidia kuepukana na athari za njaa kutokana na mazao kukauka na wengine kushindwa kulima.

"Kulivyotokea hii sintofahamu ya mvua kutokunyesha kwa miezi hii ndipo diwani akatukusanya sisi wananchi na watumishi kutoka madhehebu mbalimbali kwa pamoja tukae ili tuweze kupeleka haja zetu mbele ya Mungu," alisema Monica.

Frank Ulendo alisema wameaathirika kisaikolojia kwa sababu mvua hakuna na wameshindwa kuhudumia mashamba kwa sababu ardhi aina unyevunyevu.

Naye Mchungaji wa Kanisa la EAGT, Fesoni Sanga, alisema kabla ya maombi hayo na wananchi wao walianza maombi ya kufunga kwa siku tatu, huku wakiwataka wananchi kuachana na imani potofu za kuamini kuwa mvua hiyo inazuiliwa na baadhi ya watu.

Diwani wa Kata ya Utengule, Stephano Mgoba alisema wamelazimika kufanya maombi hayo ili kuondoa imani potofu kwa baadhi ya wananchi ambao wamekuwa wakiamini kuwa ukame huo umesababishwa na miradi ya kiuchumi inayotekelezwa na serikali.

Aliitaja miradi hiyo ni ujenzi wa kiwanda cha nondo na machimbo ya madini yanayoendelea katika Kata ya Mtwango.

Sadaka ambazo zimepatikana katika ibada ya maombi hayo ya kuombea mvua zimeelekezwa kusaidia wenye mahitaji maalumu na watoto yatima.



## Serikali yataja lengo mfumo utoaji huduma za serikali

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar, Dk. Seif Said Seif, amesema mfumo wa utoaji huduma za serikali kupitia sehemu moja umelenga kufikia serikali ya kidijitali.

Aliyasema hayo wakati wa hafla ya utoaji mafunzo kwa masheha wa Wilaya ya Mjini kuhusu mfumo wa kidigitali wa eDUA ambao ni jukwaa la kidigitali linaloleta huduma za kidigitali kwa pamoja serikalini uliofanyika katika Ofisi za EGAZ Michenzani Zanzibar.

Alisema hatua hiyo imelenga kuondoa utumiaji wa karatasi na mwananchi anapotaka huduma za kijamii ikiwamo sherehe za harusi au msiba kuomba kibali kupitia njia ya mtandao.

Mkurugenzi Seif alisema ni imani yake masheha hao watakuwa chachu ya nchi kubadilika kutoka sehemu moja kwenda nyengine.

"Tunaamini mabadiliko hapa Zanzibar yanawezekana na tunaamini mfumo huu na mengine itasaidia wananchi kupata huduma za kiserikali sehemu moja lengo ni kuona TEHAMA inaonekana umuhimu wake kwa mwananchi wa kawaida na hata kwa wageni wanaokuja Zanzibar," alisema.

Hata hivyo, alibainisha kuwa wameanza kwa masheha wa Wilaya ya Mjini na baadaye mafunzo hayo yatakuwa endelevu kwa masheha wote wa Unguja na Pemba ili kuona mfumo huo unafanikiwa.

Alisema ushirikiano huo utawezesha kuleta mafanikio ya haraka kwa Zanzibar katika kuelekea serikali ya kidijitali na malengo yaliyowekwa kufikiwa kwa haraka na kwa ufanisi mkubwa.

Akifungua mafunzo hayo Mkuu wa Wilaya ya Mjini, Hamid Seif Said alisema utumiaji wa mifumo ya kidigitali inayoanzishwa serikalini itasaidia kwa kiasi kikubwa kuondoa rushwa na kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Alisema hatua hiyo ya kuanzishwa kwa mifumo ya kidigitali serikali ni hatua muhimu katika kupambana na rushwa na kuboresha huduma bora kwa umma.

Aidha, alisema kuja na mfumo huo na kuwa na mlango mmoja wa huduma pia itasaidia kwa kiasi kikubwa kuondoa changamoto zinazowakabili wananchi na kurahisisha ufanisi wa masheha katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

Alitumia nafasi hiyo kuwataka masheha kubadilika na kufikia azma ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi kwenda kidigitali na utoaji wa huduma serikalini zinakuwa rahisi na haraka.

Naye Meneja wa mtandao wa simu Mixx by Yas Zanzibar, Salum Nassor Mohamed, alisema kampuni hiyo ikishirikiana na serikali kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi kuchangia huduma za serikali kutumia simu zao za mkononi.

Saleh Salum Othman ambaye ni mtaalamu wa mfumo huo alisema dunia hivi sasa inakwenda kidijitali na mara nyingi wakiendesha huduma kwa njia ya makaratasi.

Aidha, alisema hivi sasa serikali inaondoka katika kutoa huduma kwa njia ya makaratasi na kutumia mtandano ili kurahisisha utoaji wa huduma mbalimbali kwa wananchi wa Zanzibar.

# Malezi ya watoto Z'bar bado tatizo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Abeda Rashid, amesema kuwa Zanzibar kuna changamoto kubwa ya malezi kwa watoto, hivyo ni vyema kuwa na sera ya ustawi wa jamii.

Aliyasema hayo juzi katika kikao cha kujadili mwongozo wa sera ya ustawi wa jamii kilichowashirikisha wadau mbalimbali.

Abeda alisema wameona Zanzibar kuna haja ya kuwa na mwongozo wa sera ya ustawi wa jamii ili kuwa na mwelekeo mzuri wa kusimamia maendeleo ya ustawi wa jamii.

Alisema sera hiyo itagusa mambo mengi ikiwamo masuala ya teknolojia, uwezeshaji wanawake kiuchumi, afya, malezi na elimu.

Alisema rasimu ya sera ya maendeleo ya jamii itagusa kila eneo ili utekelezaji wa sera hiyo kumgusa kila mwananchi.

Katika hatua nyingine alisema kuwapo kwa ushirikiano kati ya Wizara na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru itasaidia kukuza maendeleo kwa jamii wa pande zote mbili za muungano.

Akizungumza katika hafla ya utiaji saini hati ya ushirikiano baina ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru alisema lengo la ushirikiano ni kuwajengea uwezo watendaji wa wizara na Taasisi ya Tengeru kufanya utafiti mbalimbali zitakazosaidia kutoa mwelekeo wa namna ya kuwatumikia jamii na kuleta mabadiliko.

Alisema ushirikiano huo utasaidia kufanya programu mbalimbali za miradi ya maendeleo ili kubadilisha mitizamo ya watu juu ya kuifikia miradi ya maendeleo.

Alisema bado Zanzibar inahitaji wataalamu wa ngazi ya jamii na Chuo cha Tengeru kinauzoefu wa muda mrefu wa kutoa taaluma ya maendeleo ya jamii na tayari kimeshatoa wataalamu wengi.

Alisema kuwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii imepewa dhamana kubwa ya kusimamia na kuimarisha maendeleo ya jamii, hivyo kuwapo kwa ushirikiano huo kutaisaidia wizara kutekeleza jukumu hilo kwa urahisi.

Mkuu wa Chuo cha Tengeru, Dk. Bakari George alisema mchakato wa kuanzisha mashirikiano umechukua takribani mwaka mmoja, hivyo aliwashukuru kwa kukamilisha mchakato huo ambao utaleta tija kwa wanajamii.

Alisema Tengeru ni chuo chenye uzoefu wa miaka 60, hivyo watahakikisha ushirikiano huo unaleta tija kwa wananchi wa Zanzibar na Tanzania Bara.

Alisema hati hiyo inaangalia zaidi kubadilishana uzoefu katika maeneo ya sera ya maendeleo ya jamii ili kuisaidia serikali katika kuwaletea maendeleo wananchi.

Aidha, alisema taaluma ya maendeleo ya jamii imekuwa hasa katika nchi zilizoendelea na Chuo cha Tengeru inahakikisha kinakwenda na mabadiliko ya kidunia ili taaluma hiyo iendane na hali ya sasa ya kuwawezesha wananchi kujiletea maendeleo.



Mkuu wa Wilaya ya Mjini, Hamid Seif Said (kushoto), akizungumza wakati akifungua mafunzo kwa masheha wa wilaya hiyo, katika ofisi za taasisi ya serikali mtandao EGAZ Michenzani, mjini Unguja jana, kuhusu mfumo wa kidigitali wa eDUA ambao ni jukwaa linaloleta huduma za kidigitali kwa pamoja serikalini. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Chanjo kichaa cha mbwa kuendelea kutolewa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, imesema itaendelea kutoa chanjo ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa ili kuikinga jamii na madhara yanayosababishwa na wanyama hao.

Mkurugenzi Idara ya Maendeleo ya Mifugo, Asha Zahran Mohammed aliyasema hayo huko Ndijani Mseweni wakati wa uzinduzi wa utoaji chanjo ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa kwa ajili ya kuzuia maambukizi.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina lengo la kutunza jamii yao ili kunusuru maradhi hayo yasiwapate binadamu na ndiyo maana zoezi la chanjo hiyo hutolewa bure bila ya uwepo wa malipo yoyote kwa wanyama hao," alieleza.

Alisema inapaswa kila mfugaji kuona umuhimu wa kuchanja mbwa na wanyama wengine kupitia zoezi hilo na kufanya hivyo kuhatarisha maisha ya viumbe wengine pamoja na binadamu.

Asha alisema kuwa wizara kupitia idara yake imejipanga vyema ili kutokomeza ugonjwa huo na kuhakikisha mbwa wote wanachanjwa kila mwaka kupitia zoezi kama hilo.

Alisema kwa wafugaji watakaokosa chanjo hiyo wanatakiwa kufika katika kituo cha mifugo ili wanyama wao wapatiwe chanjo hiyo.

Naye Daktari wa Mifugo, Ali Mohammed Zahran, alisema ugojwa huo hauna dawa bali unaweza kuzuiliwa kwa kutumia chanjo, kwamba ugonjwa huo ukimpata binadamu huwa hauna tiba mahsusi na huenda ukasababisha kifo.

"Kutokana na hilo ndiyo maana tunahakikisha tunatoa taarifa kwa wafugaji wa kila wilaya na kuwahimiza wafugaji wa mbwa kuwa makini hasa katika suala la chanjo ili mbwa wao waweze kuendelea kuishi vizuri na afya," alisema Dk. Zahran.

Sheha wa Ndijani Mseweni, Masoud Said Abdallah, aliwashukuru madaktari wa mifugo kwa kufika katika shehia yao na wafugaji wengi waliopo katika eneo hilo wamewachanja.

Baadhi ya wafugaji walioshiriki zoezi hilo waliishukuru serikali kwa kuwaletea chanjo hiyo na kuwataka wafugaji wenzao kuwafikisha katika vituo vya kutolea chanjo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**MANSON LISLOT KIVAMBA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1667/0100** kilichotolewa na Irole Secondary School mwaka 2009. Cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P4050/0405** kilichotolewa na Retco Education Center mwaka 2011. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/IRI/KIL/1005/2025.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**DAUDI ELIUDI NTUNDA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S3895-0066** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **IPEMBE SECONDARY SCHOOL** mwaka 2021. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/SIN/SIN/585/2025.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya CHALINZE Wilaya ya BAGAMOYO**

**Mdai: MOHAMED OMARY MAGOMA**

**Mdaiwa: ALLY MAHADHI JUMA**

**Kwa: ALLY MAHADHI JUMA**

**Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba**
**UNATAKIWA KUFIKA MAHAKAMANI BILA KUKOSA**

Kwa hiyo unahitajiwa/mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya JUMATANO tarehe 12 mwezi 02/2025 saa 03:00 asubuhi kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO** kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama hii leo t**arehe 16 mwezi 01/2025.**

HAKIMU MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO
CHALINZE-BAGAMOYO

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJ

**KASSIM ABDUL MAMBA**

anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaj yenye namba za usajili **MC 748 CPF – TVS KING.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/NJO/NJO/421/2025.**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**KASSIM ABDUL MAMBA**

anatangaza kupotelewa na kadi ya BAJAJI yenye namba za usajili **MC 696 CQZ - TVS KING.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/NJO/NJO/421/2025.**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**(HATI YA WITO MBELE YA TUME YA USULUHISHI NA UAMUZI)**
**((Made under Regulation 34((1))(Imetengenezwa chini ya Kanuni ya 34((1)).**
**Labour Dispute No. (Mgogoro wa kikazi Na.)**
**CMA/DSM/KIX/608/2024**
**Between/baina ya**
**FABIAN WILBALD MSOFE......................Applicant (Malalamikaji/mwombaji)**
**And/na**
**TRACE INCORPORATION COMPANY LIMITED................Respondent (Mlalamikiwa/mjibu maombi)**
**NOTICE TO ATTEND MEDIATION/ARBITRATION HEARING**
**TAARIFA YA KUITWA KUHUDHURIA KWENYE SHAURI LA USULUHISHI/UAMUZI**

Take notice that the above mentioned mediation arbitration has been fixed for hearing 03 day of February year 2025 at 10:00 am hours at DAR ES SALAAM ZONE, AKIBA-BIBI TITI ROAD (unaarifiwa kuwa shauri lililotajwa hapo juu linakuja kwa hatua ya usuluhishi/uamuzi, limepangwa kusikilizwa tarehe...........mwezi........... mwaka 2025 saa............... mahali KANDA YA DAR ES SALAAM, BARABARA YA AKIBA-BIBI TITI.

You are required to appear before the Commission in person and or accompanied by an Advocate Personal representative at instructed and produce on that day all relevant documents you intend to rely upon in support of

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**LA WILAYA YA KONDOA**
**MAHALI KONDOA**

**SHAURI LA MADAI Na. 67 MWAKA 2024**

**FATAA SAID........................................................ MDAI**

**DHIDI YA**

**1. ISSA JANI........................................................ MDAIWA**
**2. HALIDI SIMBA....................................................MDAIWA**
**3. ANAFI NKURO....................................................MDAIWA**
**4. HUSSENI OMARI................................................MDAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

**KWA: ISSA JANI, HALIDI SIMBA, ANAFI NKURO NA HUSSENI OMARI**

**POPOTE MLIPO.**

Kwa kuwa mdai aliyetajwa hapo juu amefungua Shauri la Maombi/Madai ya Eneo la Shamba dhidi yenu.Shauri ambalo maelezo yake yameelezwa katika Nakala za Hati ya Maombi inayopatikana katika Mahakama/Baraza hili kwa hiyo mnatakiwa kuhudhuria ninyi wenyewe au Wakili au Mwakilishi wenu anayeruhusiwa kisheria ,siku ya tarehe 23/1/2025 saa 3.00 kamili Asubuhi bila kukosa mbele ya Mheshimiwa R.S.MANDARI.Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya.Kwa ajili ya kujibu Maombi/Madai haya dhidi yenu.

**ANGALIZO:** -Kama msipohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama/Baraza ikithibitisha kuwa mlipokea taarifa hii ya kuitwa kwa hili Shauri basi shauri linaweza kusikilizwa na kutolewa hukumu bila uwepo wenu.Mnaagizwa kuleta vielelezo vyote ambavyo ambavyo vinatakiwa katika utetezi wenu siku hiyo.

Wito huu umetolewa kwa amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza/Mahakama Leo Tarehe 19,Mwezi Desemba Mwaka 2024.

..........................................................
**R.S.MANDARI**
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA**

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MASJALA NDOGO YA TEMEKE**
**(TEMEKE KITUO CHA JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)**

**MIRATHI NA 830 YA MWAKA 2025.**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**MALEKSULTAN ESSA KASSAM**

**NA**

**ALKARIM SHAMSHUDIN HIRJI...........MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua ya usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 24 mwezi Februari, 2025 saa 12:30 Mchana. Siku ambayo shauri hili limepangwa kusikilizwa mbele ya **Mhe. Jaji S.D. MWAIPOPO.**

Imesainiwa Dar es salaam, leo tarehe 17 mwezi Januari, 2025.

NAIBU MSAJILI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

**SHAURI LA GHARAMA NA. 15 LA 2024**

**SHAURI NA. 58/2024**

**CECILIA KALUME....................MLETA MAOMBI**
**(Anamwakilisha Ruth M. Kalume)**

**DHIDI YA**

**SALIMU AKIDA....................MDAIWA WA KWANZA**

**KWA: SALIMU AKIDA – POPOTE ULIPO**

**CECILIA KALUME (Anamwakilisha Ruth M. Kalume)** amefungua shauri dhidi yako. Shauri husika limepangwa kutajwa tarehe 13/2/2025 saa tatu kamili asubuhi (3:00). Hivyo basi, unatakiwa kuleta utetezi wako ndani ya siku 14 kuanzia tarehe ya tangazo hili kutolewa. Vielelezo vyote vya kesi vinapatikana katika Masijala ya wazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Tanga. Endapo hutatekeleza haya, shauri hili litasikilizwa upande mmoja na Hukumu kutolewa dhidi yako.

**AMRI** hii imetolewa na kutiwa Saini Muhuri/Lakiri wa Baraza hili leo tarehe 20/1/2025.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
TANGA


***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***

***Tupigie:***

***+255 - 0677 020701***

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO,MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Amri 4 za Trump siku ya kwanza ikulu

• Imo kuiondoa Marekani WHO, kuvunjwa mkataba wa Paris

**Na Maulid Mmbaga**

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amesaini maagizo kadhaa ya rais yenye utata baada ya kuapishwa kama rais wa 47 wa nchi hiyo, akisisitiza kwamba ataleta mapinduzi katika maisha ya Wamarekani.

Rais Trump alikula kiapo mbele ya Jaji Mkuu John Roberts, huku mkewe Melania akiwa amesimama pembeni yake pamoja na Biblia.

Baada ya kuapishwa jana katika jengo la bunge nchini humo, Rais Trump alitia saini amri mbalimbali ikiwamo ya kuanza mchakato wa kuiondoa Marekani kuwa mwanachama wa Shirika la Afya Duniani (WHO).

Rais huyo mpya wa Marekani alisema jambo hilo ni kubwa, na ni miongoni mwa hatua zake za awali za utendaji alizochukua kwa siku ya kwanza madarakani.

Ilielezwa kuwa hiyo ni mara ya pili kwa Rais Trump kuamuru Marekani kujiondoa kuwa mwanachama wa WHO, huku akikosoa jinsi shirika hilo la kimataifa lilivyoshughulikia janga la Covid-19 na kuanza mchakato wa kujiondoa kutoka kwa taasisi hiyo ya Geneva wakati wa janga hilo.

Agizo hilo lilisema "Marekani inajiondoa kwa sababu ya WHO kutoshughulikia janga la Covid-19 ambalo liliibuka Wuhan, China, na majanga mengine ya afya ya ulimwengu.

"Pia kushindwa kwake kupitisha mageuzi yanayohitajika haraka, na kutokuwa na uwezo wa kuonyesha uhuru kutoka kwa yasiyofaa. Pamoja na ushawishi wa kisiasa wa nchi wanachama wa WHO," ilisema sehemu ya agizo hilo.

Amri hiyo ya utendaji pia ilisema hatua hiyo ilitokana na malipo yasiyofaa ambayo Marekani ilitoa kwa WHO, ambayo ni sehemu ya Umoja wa Mataifa (UN).

Ilibainishwa kuwa Trump alipokuwa bado ofisini kwa mara ya kwanza alikosoa shirika hilo kwa kuipendelea China katika kukabiliana na janga la Covid-19.

### MKATABA WA PARIS

Maagizo mengine yaliyotiwa saini ni kuiondoa Marekani kutoka kwenye mkataba wa mazingira wa Paris wa mwaka 2015.

Rais Trump alisema ameiondoa nchi ambayo ndiyo mtoaji mkubwa wa gesi chafuzi duniani, kutoka kwenye juhudi za ulimwengu za kupambana na mabadiliko ya tabia nchi kwa mara ya pili katika kipindi cha mwongo mmoja.

"Unafikiri Biden angeweza kufanya hivi? Sidhani," Trump aliwaambia wafuasi wake waliokuwa wakimshangilia huku akiwarushia kalamu alizotumia kusaini maagizo ya rais ya awamu ya kwanza.

Hatua hiyo inaiweka Marekani pamoja na Iran, Libya na Yemen kama nchi za pekee duniani ambazo haziko kwenye mkataba huo wa Paris wa mwaka 2015.

### UCHIMBAJI MAFUTA

Katika hatua nyingine, Rais Trump alisema kwamba Marekani itaanza tena uchimbaji wa mafuta na gesi baada ya hatua hiyo kusitishwa na rais aliyeondoka mamlakani Joe Biden.

Inaelezwa kuwa Rais Trump amekuwa akipinga mabadiliko ya tabia nchi na kudai ni hekaya tu, hatua iliyoenda sambamba na kuiondoa Marekani kwenye mkataba wa Paris.

Rais huyo pia alisaini agizo la kutangaza dharura ya kitaifa katika mpaka wa Marekani na Mexico na kusema atapeleka kikosi cha majeshi kukabiliana na uhamiaji haramu, ikitajwa kuwa suala muhimu wakati wa kampeni na lililomsaidia kupata ushindi dhidi ya Kamala Harris.

### 1,000 KUFUTWA KAZI

Amri nyingine Rais Trump alisema anapanga kuwaondoa kazini zaidi ya watu 1,000 walioteuliwa na utawala wa Rais wa zamani Joe Biden, akitangaza kuwafuta kazi wanne kwenye mtandao wa kijamii, akiwamo mpishi mashuhuri Jose Andres na jenerali mkuu wa zamani Mark Milley.

"Ofisi yangu ya utumishi wa Rais iko katika mchakato wa kuwatambua na kuwaondoa zaidi ya wateule 1,000 wa Rais kutoka kwa utawala uliopita, ambao hawaambatani na maono yetu," Trump alisema katika chapisho kupitia mtandao wake wa kijamii wa Truth.

Inaelezwa kuwa hatua hiyo imezua wasiwasi kwamba rais anapanga kuwaondoa wote walioteuliwa wakati wa utawala wa Biden na kuwaweka watu wanaoamini ajenda yake.

### 1,500 WAPEWA MSAMAHA

Kiongozi huyo pia ametoa msamaha kwa zaidi ya watu 1,500 waliopatikana na hatia au kushtakiwa kwa kuhusika na ghasia za kuyavamia majengo ya bunge mwaka 2021 na kujaribu kuzuia kuidhinisha kushindwa kwake na Joe Biden.

"Natumai wataachiwa huru leo kwa kweli," alisema Trump baada ya kusaini agizo hilo la msamaha.

Ilielezwa kuwa wanachama 14 Proud Boys na Oath Keepers, vikundi viwili vya siasa kali za mrengo wa kulia, ni miongoni mwa wale ambao hukumu zao zimebadilishwa na kiongozi huyo.

Rais Trump pia alitia saini agizo la kuiagiza Idara ya Sheria kufuta kesi zote zinazosubiriwa dhidi ya washukiwa wanaotuhumiwa katika ghasia hizo.

Januari 6, 2021 wafuasi wa Trump walivamia majengo ya Bunge wakati wabunge wakikutana kuthibitisha ushindi wa Joe Biden.

Hata hivyo, kiongozi huyo aliamuru kwamba atahakikisha wahamiaji wote haramu walioingia Marekani kinyume cha sheria watarudishwa makwao wakiwamo Wakenya 3,000.

Vilevile, alisema kuanzia jana taifa la Marekani litatambua jinsia mbili tu ambayo ni mwanaume na mwanamke.

### ALIVYOAPA

Rais Trump alikula kiapo chake akiwa ameinua mkono wake wa kulia juu, bila kuuweka mkono wake wa kushoto juu ya Biblia mbili ambazo mkewe Melania alizishikilia alipokuwa amesimama kando yake.

Shirika la Reuters, liliripoti kuwa wataalamu walisema tukio hilo halina athari yoyote kwa kiapo chake, lakini limeibua mjadala katika mitandao ya kijamii, kwa kutoweka mkono kwenye Biblia, ambayo ni maandiko matakatifu ya Wakristo na Wayahudi.

"Kile anachotumia rais ajaye kuapa, iwe ni Biblia, hati ya kihistoria au bila ya chochote, si muhimu ili kutwaa mamlaka," alisema Jeremi Suri, Profesa wa historia na masuala ya urais wa Chuo Kikuu cha Austin, Texas.


"Hakuna kitu katika katiba kinachosema rais anapaswa kuunganisha kiapo chake na Mungu kwa njia yoyote ile kiapo ni kwa katiba," alisema.

Kadhalika alisema kuwa katiba inaruhusu rais mteule kuapa au kuthibitisha, na kwamba waanzilishi wa Marekani waliliweka hilo hivyo wakijua kuna wengine wanaweza kutokea wasio amini Mungu.

Timu ya kiongozi huyo ilisema, Trump alichagua Biblia ambayo Rais wa 16 Abraham Lincoln aliapishwa nayo mwaka 1861 na Barack Obama 2009 na 2013, Bibilia nyingine ni ile ambayo alipewa na mama yake.

Licha ya Marekani kuwa na utamaduni wa kutokualika viongozi wa nchi zingine wakati wa hafla ya uapisho, hali ilikuwa tofauti kidogo siku ya Januari 20 kwani Rais wa Argentina Javier Milei na Waziri Mkuu wa Italia, Giorgia Meloni, walipata bahati ya kuhudhuria.

Hata hivyo, kama ilivyokuwa mwaka 1985 wakati wa Rais Ronald Reagan, uapisho wa Trump ulifanyika sehemu ya ndani ya majengo ya bunge kutokana na hali mbaya ya hewa. **Chanzo mtandao**



Rais wa Marekani, Donald Trump, akila kiapo mbele ya Jaji Mkuu, John Roberts. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



Rais wa Marekani, Donald Trump, akitia saini mikataba mbalimbali baada ya kuapishwa.

> "Unafikiri Biden angeweza kufanya hivi? Sidhani," Trump aliwaambia wafuasi wake waliokuwa wakimshangilia huku akiwarushia kalamu alizotumia kusaini maagizo ya rais ya awamu ya kwanza.

# TAMASHA LA SAUTI ZA BUSARA KUNOGESHWA NA WASANII 50

Na Faustine Feliciane

TAMASHA la 22 la muziki la Sauti za Busara kwa mwaka huu, limepangwa kufanyika Zanzibar kwa siku tatu kuanzia Februari 14 hadi 16, huku likitarajiwa kupambwa na wasanii zaidi ya 50 katika majukwaa manne tofauti yatakayoandaliwa, imeelezwa.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana kwenye mkutano na waandishi wa habari, Mkurugenzi wa Tamasha hilo, Journey Ramadhan, alisema ni miaka 22 sasa Zanzibar inahodhi tukio la Sauti za Busara na tayari wadau mbalimbali wamethibitisha kushiriki.

"Kwa mwaka huu kaulimbiu ni 'Voice for Peace' ikimaanisha 'Sauti ya Amani'. Tunaamini kupitia muziki tunaweza kuleta amani katika maeneo mbalimbali yenye mtafaruku kupitia ujumbe mbalimbali," alisema Ramadhan.

Aidha, alisema kwa mwaka huu kutakuwa na majukwaa manne tofauti na yote yatatumika kwa wasanii mbalimbali.

**"Tutakuwa na majukwaa mawili Ngome Kongwe, jukwaa moja Forodhani na moja Fumba City, yote haya yatatumika na wasanii mbalimbali kwa wakati mmoja kulingana na aina ya muziki," alisema.**

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Busara Promotion, Lorenz Herrman, alisema mbali na wasanii mbalimbali wa ndani na nje kupanda jukwaani, pia kutakuwa na makongamano mbalimbali.

"Tunajukumu sasa la kulipeleka tamasha hili mbali kwa miaka 20 ijayo baada ya kuanzishwa kwake na Mhasisi Yusuph Mohamed na kuweka misingi imara, tunawashukuru washirika wetu ambao wameungana na sisi.

"Tunatarajia tutakuwa na wakongamano mbalimbali ambapo wasanii watapata fursa ya kubadilishana ujuzi, lakini pia elimu ya kupinga unyanyasaji wa kijinsia itatolewa, ni fursa nzuri kwa wasanii na Watanzania kwa ujumla," alisema Herman.

Aidha, Mwenyekiti wa Busara Promotion, Simai Said, amewaomba Watanzania hususan Wazanzibar kujitokeza kwa wingi kwenye tamasha hilo pamoja na kuendelea kuonesha ukarimu wao kwa mamia ya wageni watakaofika kushuhudia tamasha hilo.

Balozi wa Umoja wa Ulaya hapa nchini, Christine Grau, alisema Taasisi ya UN Women itatumia tamasha hilo kutoa elimu juu ya kupinga unyanyasaji wa kijinsia pamoja na kuhamasisha wanawake kushiriki kwenye shughuli mbalimbali.

Mmoja wa wasanii watakaoshiriki tamasha hilo, Leo Mkanyia, alisema wamejiandaa vizuri kutoa burudani kwenye tamasha hilo ambalo litakuwa na wasanii kutoka ndani ya Afrika na nje.

Zaidi ya wasanii 50 watapanda kwenye majukwaa hayo kutoa burudani huku kwa Tanzania, msanii Frida Aman atakuwa miongoni mwa watakaoshiriki pamoja na vikundi vingine kutoka Zanzibar.



Wachezaji wa Tabora United wakifanya mazoezi kuelekea mechi yao ya kiporo ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Simba itakayochezwa Februari 2, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani Tabora. **NA MPIGAPICHA WETU**

# JKT Tanzania yaota michuano CAF

Na Somoe Ng'itu

UONGOZI wa JKT Tanzania umeanza mikakati ya kuhakikisha timu yao inafanya vizuri na hatimaye kukata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), katika msimu ujao, imeelezwa.

Ofisa Habari wa JKT Tanzania, Masau Bwire, alisema jijini Dar es Salaam jana, wamejipanga kufanya vema katika mechi za mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Bara kwa sababu wanataka kushiriki michuano ya kimataifa na hiyo ndio njia pekee ya kufikia malengo yao.

Bwire alisema baada ya kupoteza malengo ya awali ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, sasa watahakikisha wanapata matokeo chanya katika mechi za mzunguko wa pili na kukata tiketi ya kushiriki michuano ya CAF msimu ujao.

"Kwa kabisa malengo ya timu huwa ni kushinda kile mnachokiwania, lakini ikitokea hilo haliwezekani, basi mnakwenda katika malengo yanayofuata, nayo ni kuhakikisha tunafanya vizuri katika mechi za lala salama na hatimaye kukata tiketi ya kushiriki michuano ya CAF, tunaamini hili tutafanikiwa," alisema Bwire.

Aliongeza kuwa benchi la ufundi la timu yao linaendelea kutumia vema muda huu ambao Ligi Kuu Tanzania Bara imesimama kurekebisha mapungufu ili watakaporudi dimbani wawe tayari kukabiliana na ushindani.

"Tunataka kuonesha ubora wetu katika mzunguko wa lala salama ili kufikia malengo tuliyonayo, tunajua haitakuwa rahisi kwa sababu kila mmoja anahitaji kufikia malengo yake, sisi kwa upande wetu tunataka kuendeleza kichapo cha kizalendo," aliongeza Bwire.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Bara, Maafande hao wa JKT Tanzania wako kwenye nafasi ya nane wakiwa na pointi 19 kibindoni, wamecheza michezo 16, wameshinda minne, sare saba na walikubali kichapo mara tano.

Simba yenye pointi 40, lakini ikicheza michezo 15 ndio vinara wa ligi hiyo ikifuatiwa na Mabingwa Watetezi, Yanga wenye pointi 39, Azam FC yenye pointi 36 iko katika nafasi ya tatu na 'TOP 4' inakamilishwa na Singida Black Stars yenye alama 33.

Ligi Kuu Tanzania Bara itarejea Februari Mosi kwa Yanga kuwakaribisha Kagera Sugar kwenye Uwanja wa KMC wakati kesho yake Simba watakuwa ugenini kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani, Tabora kuwavaa wenyeji, Tabora United.

## Kipa wa Simba ajiunga rasmi na Kagera Sugar

Na Adam Fungamwango

KLABU ya Kagera Sugar imemsajili kipa namba nne wa Simba, Ahmed Feruzi kwa ajili ya kuitumikia timu hiyo kwenye hatua ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Taarifa iliyotolea jana na klabu hiyo, imeeleza, Feruzi atakuwa mmoja kati ya wachezaji wa timu hiyo ambao haijafanya vema kwenye mzunguko wa kwanza.

"Tunamkaribisha mwana familia mpya, Feruzi kwenye timu bora Ukanda wa Ziwa Victoria, akitokea Klabu ya Simba," ilieleza taarifa hiyo kutoka Idara ya Habari na Mawasiliano.

Hata hivyo, taarifa kutoka ndani ya Simba zinaeleza kuwa mchezaji huyo amepelekwa kwa mkopo wa miezi sita ili kulinda na kuendeleza kipaji chake.

"Ni kipa wetu mzuri sana, lakini bado mdogo na kuna makipa wengi wazuri, wazoezi na wenye ubora juu yake, hivyo tumeamua kumpeleka sehemu nyingine ambako atapata nafasi ya kucheza kwa ajili ya faida ya baadaye yake mwenyewe, Simba na timu ya taifa," kilisema chanzo kutoka ndani ya Klabu ya Simba.

## Singida yasitisha kambi Arusha

Na Adam Fungamwango

KLABU ya Singida Black Stars, imetangaza kusitisha kambi yake ya mwezi mzima iliyopangwa kuifanya jijini Arusha, badala yake wanarejea mkoani Singida kujiandaa na Ligi Kuu Tanzania Bara, inayotarajiwa kuendelea tena, Ferbruari Mosi, mwaka huu.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Hussein Masanza, alisema jana kuwa kusitishwa kwa siku za kuendelea kukaa kambini kunatokana na mabadiliko ya ratiba ya Ligi Kuu, ambapo awali ilikuwa irejee, Machi Mosi, lakini imerudishwa nyuma, hivyo wanavunja kambi jijini Arusha na kurejea Singida kwa maandalizi ya mwisho kabla haijaanza.

"Bado tupo Arusha, awali tulipanga tukae takriban mwezi mzima, lakini baada ya taarifa za ligi kurejea Februari, tumeamua kusitisha kambi yetu kwa muda huo na sasa tutarudi Singida, ili kupata muda wa kufanya maandazili ya mwisho, ikiwamo kucheza mechi za kirafiki angalau mbili tu," alisema.

Timu hiyo inashika nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu, ikiwa imekusanya pointi 33 kwa michezo 16 iliyocheza mpaka sasa, ikishinda mechi 10, sare tatu na kupoteza mitatu, ikifunga mabao 22 na kuruhusu 11 kwenye wavu wake.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### GERNACHO ATAKIWA NAPOLI

KLABU ya Napoli ina matumaini ya kufikia mkataba wa pauni milioni 50 kumsajili winga wa Manchester United na Argentina, Alejandro Garnacho, 20. ***(Corriere dello Sport)***

### VILLA YAKATAA KWA DURAN

WEST Ham la kumsajili Jhon Duran kwa pauni milioni 57 limekataliwa na Aston Villa, ambao wameamua kutomuuza mshambuliaji huyo wa Colombia mwenye thamani ya pauni milioni 80 katika kipindi hiki cha dirisha dogo la uhamisho wa wachezaji. ***(Telegraph)***

### DORGU AWANIWA UNITED

KLABU ya Manchester United inajadiliana na beki wa Lecce, Patrick Dorgu, kwa lengo la kumsajili mchezaji huyo wa Kimataifa wa Denmark, 20, ili kuziba pengo katika kikosi cha Ruben Amorim. ***(Athletic)***

### AIT-NOURI AFUATILIWA

MANCHESTER United pia inamfuatilia beki wa Wolves, Rayan Ait-Nouri, 23, na beki wa Crystal Palace na England, Tyrick Mitchell (25), kwa kuhofia kumkosa mlinzi wa Paris-St Germain na Ureno, Nuno Mendes, 22, katika uhamisho wa wachezaji Januari hii. ***(ESPN)***

### ANCELOTTI KUMPISHA ALONSO

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, anatarajiwa kuondoka katika klabu hiyo majira ya joto, huku Kocha wa Bayer Leverkusen, Xabi Alonso, akipigiwa upatu kuchukua nafasi ya Muitaliano huyo. ***(Ondacero)***

### KANOTE NA MKATABA

LIVERPOOL inakabiliwa na mgogoro mpya wa mkataba, huku beki wa Ufaransa, Ibrahima Konate, 25, akiwa bado hajatia saini mkataba mpya na klabu hiyo licha ya kupewa ofa mpya. ***(Telegraph)***

### GREALISH AWANIWA INTER

KIUNGO wa Manchester City na England, Jack Grealish, 29, ananyatiwa na Inter Milan na Borussia Dortmund, huku mustakabali wake Etihad ukizidi kutofahamika. ***(Sun)***

### DELAP AFIKIRIWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inafikiria kumnunua mshambuliaji wa Ipswich Town, Liam Delap, 21, mwezi huu, lakini huenda wakakabiliana na ushindani kutoka kwa Chelsea. ***(Team Talk)***

### ELLIOTT HAUZWI

LIVERPOOL haina nia ya kupokea dau la kumuuza kiungo wa kati wa England, Harvey Elliott, 21, katika dirisha hili la Januari au katika uhamisho wa majira ya joto, licha ya kukosa kukichezea kikosi cha kwanza. ***(Football Insider)***

### UNITED KUMKOSA KERKEZ

MLINZI wa Hungary, Milos Kerkez, 21, atabakia Bournemouth licha ya kuwaniwa na Manchester United, lakini mchezaji huyo huenda akahama wakati wa majira ya kiangazi. ***(Florian Plettenberg, Sky Germany)***

## DONDOO ZA MAGAZETI YA



# VINICIUS JR AWATOA UDENDA WASAUDIA

**RIYADH,** Saudi Arabia

### Ancelotti aweka ngumu, asema wana mradi wao na wamepoteza wachezaji muhimu, hivyo...

MFUKO wa Uwekezaji wa Umma wa Saudi Arabia unaendelea kuonesha nia ya kutaka kumsajili Vinicius Junior kutoka Real Madrid, kwa mujibu wa ripoti.

**Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, ambaye alimaliza mshindi wa pili mbele ya Rodri kwenye tuzo ya Ballon d'Or mwaka jana na baadaye kutawazwa Mchezaji Bora wa FIFA, aliripotiwa kuwa analengwa na klabu moja ya Ligi Kuu ya Saudia msimu uliopita.**

Khaled Al Issa, Mkurugenzi wa Al Ahli, baadaye alithibitisha kwamba klabu yake ilikuwa na nia ya kumsajili Vinicius baada ya kumruhusu Allan Saint-Maximin ajiunge na Jose Mourinho kule Fenerbahce.

Lakini baadaye iliwalazimu miamba hao wa Saudia kumsajili mshambuliaji wa Brentford, Ivan Toney badala yake.

ESPN iliripoti kuwa mawasiliano yalianzishwa tena kati ya klabu hiyo na wawakilishi wa Vinicius Desemba, na wameonesha kwamba Mbrazil huyo anabakia kuwa mojawapo ya vipaumbele vyao vya juu kwa usajili.

"Hakuna kitu kabisa," alisema Kocha wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, wakati huo kuhusu uwezekano wa Vinicius kuondoka.

"Bila shaka uvumi haumwathiri Vinicius. Yupo hapa, anataka kuwa hapa. Anataka kufanya kila awezalo na kuisaidia Real Madrid.

"Tuna mradi wetu na tunaendelea katika hilo. Tuna kikosi cha ubora wa hali ya juu. Tumepoteza wachezaji muhimu na tumeleta wengine ambao wanapaswa kubadilika. Tunapaswa kufanya kazi ili kudumisha hali ya hewa na kujitolea."

Vinicius alikuwa na mchango mkubwa kwa Real Madrid kushinda taji la 15 la Ligi ya Mabingwa Ulaya, wakati mabao yake 15 ya LaLiga yaliisaidia klabu hiyo kutwaa taji la 36 mbele ya wapinzani wao, Barcelona.

Alizungumza juu ya nia yake ya kubakia hapo kwenye dimba la Santiago Bernabeu katika miaka ijayo wakati wa hotuba yake ya tuzo ya Mchezaji Bora wa mwaka wa FIFA, alisema anawachukulia wababe hao wa Hispania kuwa msingi wake na anataka kuendelea kucheza pamoja na Kylian Mbappe na Jude Bellingham.

Kwa upande wa Saudia wanaendelea kujivunia majina ya wachezaji kama Cristiano Ronaldo na Karim Benzema, na wana nia ya kumpata Mohamed Salah kwa uhamisho wa bure msimu huu wa majira ya joto ambapo mkataba wake na Liverpool utakuwa umefikia ukingoni.

HABARI MICHEZO

# AC MILAN YAJITOSA KWA JOÃO FELIX




**MILAN,** Italia

AC Milan inafikiria kumsajili kwa mkopo João Felix wa Chelsea na wachezaji wawili wa Manchester United, Joshua Zirkzee na Rasmus Højlund, baada ya kukubali kushindwa katika harakati zao za kumnasa Marcus Rashford, kwa mujibu wa ESPN.

Mshambuliaji wa Feyenoord na Mexico, Santiago Gimenez analengwa na Milan kwa uhamisho wa kudumu iwapo beki wa England, Fikayo Tomori atauzwa mwezi huu.

Milan walikuwa wamemwekea fowadi wa United na England, Rashford kama chaguo lao kubwa la kumpeleka San Siro kwa mkopo baada ya mazungumzo na kambi ya mchezaji huyo na United.

Lakini kwa mujibu wa ESPN, sasa Milan imekubali kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, anasubiri chaguzi nyingine baada ya kuweka wazi kwamba anapendelea kuhamia Barcelona.

Huku Rashford akikataa nafasi ya kuhamia klabu hiyo, Milan sasa iko tayari kukamilisha dili la mlinzi wa Manchester City, Kyle Walker, ili kujaza nafasi yao moja iliyosalia kwa mchezaji ambaye si mwanachama wa Umoja wa Ulaya.

Lakini baada ya kumkosa Rashford, Milan inaendelea kuwa sokoni kutafuta mshambuliaji na vyanzo vimesema kuwa klabu hiyo inachunguza uwezekano wa kumsajili mmoja kati ya Felix, Zirkzee au Højlund.

Mshambuliaji wa Ureno, Felix alikamilisha uhamisho wa pauni milioni 46.3 kutua Stamford Bridge akitokea Atletico Madrid Agosti mwaka jana, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 ameichezea Chelsea mechi 19 tu msimu huu na kucheza dakika 90 katika mchezo mmoja tu wa Ligi Kuu England.

Vyanzo vimesema kuwa fowadi huyo wa zamani wa Benfica na Barcelona ndiye chaguo linalopendekezwa na Milan baada ya kushindwa kumsajili Rashford, lakini pia kuna nia ya Zirkzee na Højlund kutokana na kuwa tayari United kufanya makubaliano mwezi huu katika juhudi za kuimarisha kikosi cha Kocha Ruben Amorim.

Zirkzee na Højlund walihamia United baada ya kufanya vema kwenye Serie A wakiwa na Bologna na Atalanta, lakini washambuliaji hao wawili wamekuwa na wakati mgumu wa kufunga kwenye Ligi Kuu England.

## Fabregas amkataa Fati

**COMO,** Italia

KOCHA wa Como 1907, Cesc Fabregas, amesisitiza kuwa hakuna ukweli wowote kuhusu uvumi unaohusisha timu yake kumtaka winga wa Barcelona, Ansu Fati, mwezi huu.

Fati anatarajiwa kuondoka Barcelona kabla ya dirisha la usajili la Januari hii kufungwa baada ya kukosa nafasi chini ya Kocha, Hansi Flick.

Como, inayoongozwa na kiungo wa kati wa zamani wa Barcelona, Fabregas, ilitajwa kuwa inamwania mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, lakini timu hiyo ya Serie A inaonekana kutokuwa na nia tena.

"Kuna baadhi ya wachezaji vijana wataondoka na tayari wanajua hilo, lakini tutawaleta wengine," alisema Fabregas.

"Hatuna mpango wa kusajili mshambuliaji.


"Niliulizia kuhusu Ansu Fati miezi sita iliyopita, lakini hakuna kitu kwa sasa."

Mshahara mkubwa wa Fati ambaye analipwa pauni 200,000 umekuwa kikwazo kwa Barcelona kumtoa kwa mkopo, kwani watalazimika kuchangia, hivyo wanataka kumuuza jumla kabla ya Februari.

Timu mbili za West Ham United na Tottenham Hotspur zimehusishwa, huku kukiwa na ripoti za kutakiwa na Real Betis.

Fati alitumia msimu wa 2023/24, kwa mkopo katika Klabu ya Brighton & Hove Albion, lakini alishindwa kujiimarisha kama mchezaji wa kikosi cha kwanza chini ya Kocha, Roberto De Zerbi.





# Konate: Nipo tayari kuifia Liverpool

**LIVERPOOL,** England

MLINZI wa Liverpool, Ibrahima Konate, amesema "nipo tayari kufa" kwa klabu hii, na amekiri kucheza kwa maumivu ili kuisaidia timu yake kutwaa Ubingwa wa Ligi Kuu England msimu huu.

Konate alikuwa nje ya uwanja kwa zaidi ya mwezi mmoja baada ya kupata jeraha la goti wakati Liverpool ikishinda mabao 2-0 dhidi ya Real Madrid Novemba mwaka jana, na kurejea kwenye kikosi cha kwanza kwenye sare ya 2-2 na Manchester United mapema mwezi huu.

"Nilijaribu kurejea kwa asilimia 100, lakini haikuwa sawa kwa sababu niliharakisha kurudi uwanjani," alisema Konate katika mkutano na waandishi wa habari jana.

"Nimefanya hivi kwa ajili ya timu yangu, naweza kufa kwa ajili ya timu hii, najua nitapona goti langu kwa asilimia 100 hivi karibuni, bado nina maumivu, nacheza na dawa za kutuliza maumivu.

"Nilikuwa karibu sana kurudi. Mpango wangu ulikuwa ni kufanya mazoezi wiki hiyo, lakini nilipomwona Joe Gomez akiwa na jeraha nilisema: 'Sawa, lazima nirudi haraka.'

"Kwa hakika, mchezo wa kwanza nilihisi goti langu kidogo, lakini inakuwa bora siku baada ya siku madaktari na wahudumu wa afya wamenifanyia kazi nzuri."

Konaté amekuwa mchezaji bora chini ya kocha Arne Slot, akiisaidia Liverpool kupata uongozi wa pointi sita kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu England.

Alipoulizwa kama anaamini yeye na Virgil van Dijk ndio mabeki bora wa beki wa kati barani Ulaya, mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ufaransa alisema: "Kwa msimu huu ndiyo. Kila mtu anamjua Virgil, kila mtu anajua ubora wake.

"Kwangu yeye ni bora zaidi hakuna aliye bora zaidi yake katika nafasi hii, sijawahi kumwambia ila natamani kuwa bora zaidi yake hata siku moja ila nataka tu kufanya bidii ili siku moja nifikie kiwango hicho."

## Mo atoa neno...

INATOKA UK. 24

Tabora United unaotarajiwa kupigwa Februari Mosi, mwaka huu, katika Uwanja Ali Hassan Mwinyi mjini Tabora.

Meneja Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, amesema macho na hesabu zao wanazielekeza zaidi kwenye mchezo huo wa Februari Mosi dhidi ya Tabora United.

Alisema wanauchukuliwa kwa uzito mkubwa mchezo huo na watakwenda kwa tahadhari zote.

"Tunakwenda kukabiliana na Tabora United, haitokuwa mechi nyepesi hata kidogo, lakini tutakwenda kwa ajili ya kupata matokeo mazuri. Sijajua ubora wa Tabora United uko wapi, ila ninachojua wanaweza kushinda michezo migumu, na kama ni hivyo hata sisi tunawajibika kwenda kwa tahadhari kubwa ili wasije kupata pia ushindi mbele yetu," alisema.

Tabora United ilipata ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Yanga, Novemba 7, na kisha kulazimisha sare ya mabao 2-2 dhidi ya Singida Black Stars Novemba 25, kabla ya kuichapa Azam FC 2-1, Desemba 13, mwaka jana.

Alisema kwa hali ambayo ligi imefika hawapaswi kudondosha hata pointi moja, hivyo hawako tayari kupoteza mchezo huo.

"Katika ligi hii ilipofika ukiruhusu hata kupoteza pointi moja umesharuhusu mpinzani wako akufikie na kukupita kwa hiyo tunawajibika kuifunga Tabora na ni moja ya michezo migumu tuliyonayo mwezi Februari," alisema Ahmed.

## Yanga yaanika...

INATOKA UK. 24

wa upande wao.

Alisema kuondolewa kwenye mashindano hayo kusitoe nafasi ya mashabiki kujigawa na kuiacha timu yao bali waendelee kuungana na kujipanga kwa ajili ya msimu ujao wa mashindano ya kimataifa.

"Tulifanya kila liwezekanalo, lakini kama tulivyoona hatukuwa na bahati na wenzetu (MC Alger), wamepata nafasi ya kusonga mbele, nawaomba mashabiki wa Yanga kuendelea kuisapoti timu yao kwa ajili ya mashindano ya Ligi Kuu na Kombe la FA tuweze kutetea ubingwa wetu.

"Najua mashabiki wengi wameumia kuondolewa kwenye mashindano ya CAF, hili limetuuma sote, lakini ndio mpira ulivyo, kuanzia sasa tutajipanga kuhakikisha tunarejea kwa nguvu msimu ujao wa mashindano haya," alisema Hersi.

# SIMBA QUEENS YATAMBA KUENDELEZA UBABE TWPL

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu ya Wanawake nchini (TWPL), Simba Queens, wanatarajia kuikabili Mlandizi Queens, katika mechi ya ligi hiyo itakayochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam leo.

**Mechi hiyo ambayo awali ilipangwa kuchezwa kwenye Kituo cha TFF Kigamboni saa 10:00 alasiri jana, sasa itachezwa leo kuanzia saa 8:00 mchana.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Yussif Basigi, alisema kila mechi kwao ni kama fainali na wamejiandaa kupambana kuhakikisha wanapata pointi tatu.

Basigi alisema ligi hiyo inaushindani na ili timu yako ifikie malengo, inahitaji kushinda kila mchezo kwa ajili ya kujiimarisha katika msimamo.

"Tuko tayari kwa mechi ya kesho (leo), ninajua utakuwa mchezo wenye ushindani, ni wazi kila timu ilitumia muda wa mapumziko kujiimarisha, wakati wote mechi za mzunguko wa pili huwa ni ngumu kwa sababu ni wakati wa kurekebisha makosa ya nyuma, na ukitaka ubingwa ni lazima ushinde mechi zako," alisema Basigi.

Aliongeza kuwa anafurahia kuona ushindani unaongezeka katika kikosi chake kwa sababu kila mmoja anataka kupata namba kwenye kikosi cha kwanza.

"Lakini kutafuta nafasi ya kuitwa katika timu za taifa ni jambo linalosaidia kukuza viwango, wachezaji wanafahamu umuhimu wa kuchezea timu za taifa, kwetu ni jambo zuri na linasaidia kutupa matokeo chanya katika michezo ya ligi ya hapa Tanzania, tunaamini tutazidisha kujituma ili kutetea ubingwa," Basigi alisema.

Simba Queens ndio vinara wa ligi hiyo wakiwa na pointi 25, wakifuatiwa na JKT Queens yenye pointi 22, lakini imecheza mchezo mmoja pungufu wakati Mlandizi Queens inaburuza mkia ikiwa na pointi moja.

Wakati huo huo, Yanga Princess, imeendelea kuimarisha kikosi chake kwa kutangaza kumsajili Mchezaji Bora wa Ligi Kuu ya Wanawake Kenya msimu uliopita, Lidya Akoth.

"Tunapenda kutangaza rasmi Lidya Akoth ni Mwananchi," taarifa rasmi katika ukurasa wa Yanga Princess, ilisema.

Katika hatua nyingine, kiungo wa zamani wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars) na Simba Queens, Kadosho Shabani, amesajiliwa na Fountain Gate Princess ya jijini Dodoma.



Kikosi cha Simba Queens

# CECAFA kukutana Juba Mkutano Mkuu

**Na Somoe Ng'itu**

MKUTANO Mkuu wa mwaka wa Baraza la Soka la Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), unatarajiwa kufanyika jijini Juba, Sudan Kusini leo.

Mkuu wa Idara ya Habari na Masoko wa CECAFA, Andrew Oryada, aliliambia Nipashe jana mkutano huo utahusisha Marais na Makatibu wakuu wa nchi wanachama wa baraza hilo ambao wote wameshafika Sudan Kusini kwa ajili ya kikao hicho.

"Tunatarajia marais na makatibu wakuu wote wa nchi 12 wanachama wa CECAFA kuhudhuria mkutano huu, agenda mbalimbali zitajadiliwa, kalenda za mashindano pia zitapangwa katika mkutano huu," Oryada alisema.

Naye Msemaji wa Shirikisho la Soka la Sudan Kusini (SSFA), Albino Kuek, alisema maandalizi kuelekea mkutano huo yamekamilika na wanatarajia wajumbe wa CECAFA watashuhudia miradi mbalimbali ya maendeleo ya mchezo huo nchini humo.

"Kufanyika mkutano huu hapa kutatoa ujumbe kwa dunia kuwa Sudan Kusini ina fursa mbalimbali, kwetu hii ni sehemu ya kuonesha mapinduzi ya michezo nchini kwetu, " alisema Kuek.

CECAFA inaundwa na nchi 12 ambazo ni Tanzania Bara, Tanzania Visiwani (Zanzibar), Uganda, Kenya, Burundi, Rwanda, Ethiopia, Djibouti, Eritrea, Somalia, Sudan na wenyeji Sudan Kusini.

# Michezo

Jumatano Januari 22, 2025

Nipashe




Vinicius Jr awatoa udenda Wasaudia UKURASA 21

**CHUMA HICHO...**



Beki wa kati wa Chelsea, Tosin Adarabioyo, akiifungia timu yake bao la kuongoza wakati wakishinda 3-1 dhidi ya Wolverhampton Wanderers, kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Stamford Bridge usiku wa kuamkia jana. **PICHA: MTANDAO**

## Mo atoa neno Simba SC, hesabu kwa Tabora Utd

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Klabu ya Simba ikitangaza kuwa baada ya kumaliza mchezo wake dhidi ya CS Constantine, hesabu zote sasa zipo kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Tabora United, Mwekezaji na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Mohamed Dewji, amewapongeza wachezaji wa timu hiyo kwa kujituma uwanjani kiasi cha kufanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho.

Akitoa salamu za pongeza jana, Dewji, ambaye ni Rais wa Heshima wa klabu hiyo, alisema kikosi cha timu hiyo kinaundwa na wachezaji wengi vijana wadogo, ambao ni wapya kwenye timu, wasio na uzoefu kwenye michezo mingi ya kimataifa, lakini wamekuwa wakijituma kweli kweli uwanjani na kuipatia ushindi, wakati mwingine ukiwa ni wa kushangaza kwenye dakika za majeruhi.

"Niwapongeze wachezaji, benchi la ufundi, viongozi, wanachama na mashabiki wa Simba kwa mshikamano na mafanikio makubwa yaliyopatikana tunayoshuhudia. Mafanikio haya si kazi ya mtu mmoja ni juhudi za familia mzima ya Wanasimba wote, pamoja na serikali yetu.

"Kufuzu kwetu robo fainali ya Kombe la Shirikisho ni hatua muhimu kuelekea ndoto yetu ya kuleta taji la Afrika kwenye michezo ya kimataifa nyumbani. Tuna ndoto kubwa na tunapambana kwa bidii kuzitimiza. Lakini namalizika kwa pongezi za pekee kwa wachezaji wetu, wamekuwa wakijituma sana hadi kutufikisha hapa tulipo," alisema Mo.

Wakati huo huo, kikosi cha Simba kimepewa mapumziko ya siku nne, baada ya hapo kinatakiwa kurejea kwa ajili ya mchezo wa Kombe la FA, pamoja na Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya

INAENDELEA UKURASA 23

# Yanga yaanika ilipojikwaa CAF

**Adam Fungamwango na Faustine Feliciane**

## ●●● Yaahidi kwenda kusuka kikosi imara kurudi na nguvu mpya huku sasa ikielekeza nguvu zao kwenye...

KLABU ya Yanga imesema imepata somo na imejifunza kitu kutokana na kutolewa kwenye hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika, hivyo viongozi watakaa na kusuka mipango mipya, ili msimu ujao irejee kwa nguvu kubwa.

**Akizungumza jiijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Ali Kamwe, alisema walichojifunza ni kwamba kila siku zinavyozidi kusonga mbele inabidi nao wapige hatua zaidi na si kuwa palepale, huku michuano hiyo ikiwa migumu kila msimu.**

Alisema msimu uliopita walifuzu hatua ya robo fainali ya michuano hiyo wakiwa na pointi nane, lakini msimu huu wameshindwa wakiwa na pointi hizo.

Alisema hiyo inaonesha kila kukicha michuano hiyo inazidi kuwa migumu na inabidi kuboresha kikosi kila msimu ili kwenda na wakati.

"Funzo tulilojifunza ni kwamba kila siku zinavyozidi kusonga mbele inabidi na sisi tupige hatua zaidi, msimu uliopita tulifuzu kundi tukiwa na pointi nane, lakini msimu huu idadi hiyo hiyo ya pointi imeshindwa kutuvusha, safari hii hazikutosha, kila kukicha michuano hiyo inakuwa migumu, kuna kazi ya kufanya. Kama viongozi tutakaa na kusuka mipango vizuri ili msimu ujao turudi na nguvu kubwa," alisema Kamwe.

Aliwataka wanachama na mashabiki wa Yanga, kutulia na kuangalia mbele, huku wakijivunia mafanikio ya misimu mitatu ambayo wamefanikiwa kutinga hatua ya makundi mara tatu baada ya zaidi ya miaka 20, moja ikiwa ni kufika fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika.

"Hayakuwa matokeo mazuri kwetu, pointi nane hazikutosha kutupeleka robo fainali, haya maji yameshamwagika, yote tutakayoyazungumza, chochote tutakachokifanya kuhusu Ligi ya Mabingwa kitabakia kuwa hadithi tu, hakuna tunachoweza kukibadili kwa wakati huu.

Pamoja na hayo tunajivunia ndani ya miaka mitatu, tumecheza hatua za makundi kitu ambacho hatukuweza kukifanya kwa miaka 25, ikiwamo kutinga fainali ya Kombe la Shirikisho," alisema Ofisa Habari huyo.

Jumamosi iliyopita, Yanga ililazimishwa suluhu dhidi ya MC Alger ya Algeria kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, matokeo ambayo yaliisukumiza nje ya michuano hiyo.

Alisema kikosi hicho baada ya mapumziko, kitaanza mazoezi kesho kujiandaa na mechi za Kombe la FA, pamoja na Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Timu itarejea mazoezini keshokutwa (kesho), tuna mechi ya Kombe la FA dhidi ya Copco, ni mechi muhimu kwa ajili ya kurejesha furaha kwenye nyuso za mashabiki, tutarudi kwa nguvu kubwa," alisema.

Yanga pia inatarajiwa kushuka kwenye uwanja huo Februari Mosi, mwaka huu, kukipiga dhidi ya Kagera Sugar, ikiwa ni mechi ya kiporo cha raundi ya 16 ya Ligi Kuu.

Aidha, Rais wa Klabu hiyo, Hersi Said, amewataka mashabiki wa timu hiyo kuwa wamoja na kudumisha mshikamano licha ya kutolewa kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, alisema uongozi wa klabu hiyo pamoja na benchi la ufundi lilifanya kila jitihada za kuhakikisha timu hiyo inafuzu hatua ya robo fainali lakini bahati haiku

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >